**Mbaroni** madai ya kupandisha bei sukari



UKURASA 3

**Magari** mkweche marufuku kuingia stendi ya Mwenge

UKURASA 4



**Hatima** ya mama nyama swala sasa kujulikana Feb. 16

UK. 4



**USHINDI WA UNITED WAMVURUGA TEN HAG**

UKURASA 22


# Nipashe

Jumamosi Februari 3, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581575

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


MISWADA UCHAGUZI

# Hakuna mteremko

**•Kupita** bila kupingwa historia, Mwenyekiti, Makamu NEC kupitia usaili, Mkurugenzi aenguliwa... *Ukurasa 2*



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, akihitimisha hoja ya miswada ya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani mwaka 2023, Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa mwaka 2023 na Marekebisho wa Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 2023, Bungeni, Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Mjamzito ajifungua darajani, mtoto asombwa na mafuriko

UK. 2

UKURASA WA 24

## Simba yawaandalia mtego Mashujaa FC

WAKATI imemrejesha kikosini kiungo wake wa kimataifa kutoka Zambia, Clatous Chama, Simba inatarajia...

UKURASA 3

## Mwili mtu aliyedaiwa kutekwa wakutwa ufukweni



SACP Jumanne Muliro

**MICHEZO** YANGA YABANWA 'MBAVU' KAITABA UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan akimuapisha Doris Ntuli Kalasa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Iringa, katika Ikulu ya Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Mwenyekiti, Makamu NEC kusailiwa

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

BUNGE limepitisha miswada mitatu ya sheria iliyokuwa ikipigiwa kelele na wadau mbalimbali nchini, huku ikiridhiwa kuwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kufanyiwa usaili kabla ya kupelekwa kwa Rais kwa ajili ya uteuzi.

Sambamba na hilo, serikali imeridhia kuondolewa kwa kipengele kilichokuwa kinataka Mkurugenzi wa Uchaguzi wa NEC kuwa Katibu wa Sekretarieti ya Kamati ya Usaili.

Aidha, serikali imeridhia kifungu cha 6 (1) ambacho kilikuwa kinaweka mawanda na maudhui ya kuteua wasimamizi wasaidizi na wasimamizi wa uchaguzi, ambacho Kamati ya Bunge, ilipendekeza sheria isiweke ulazima kwa wakurugenzi kusimamia uchaguzi, hivyo kifungu hicho kifanyiwe maboresho kwa kuingiza watumishi wa umma waandamizi.

Akijibu jana hoja zilizowasilishwa na wabunge waliochangia miswada ya Sheria za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023, Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Muswada wa Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama alisema hayo yamefikiwa baada ya kushauriana na kamati.

"Baada ya kufanya consultation (kushauriana) na kamati, tumekubaliana na sisi kama serikali tumeleta proposal (pendekezo) yetu. Tumefikiri tusiache wajumbe wa tume kupitia kwenye usaili, lakini tuwe na mfumo mwingine wa kupendekeza Mwenyekiti wa Tume na Makamu Mwenyekiti wa Tume, kwa Rais ili kuteuliwa.

"Kamati inataka kuitumia kamati ya usaili na sisi tumekuja na opinion (maoni) ya kutumia viongozi wetu wakuu wa mihimili ya mahakama. Lakini wote tunakubaliana kamati ya usaili, iwasaili wajumbe wa tume.

"Katiba inamtaka Rais kuchukua hatua za kumwondoa mjumbe wa tume pale ambapo labda atakuwa amekosea. Serikali imekuja na mapendekezo ya kadiri itakavyoona inafaa, Rais anaweza kuunda kamati ya uchunguzi ili imshauri kabla ya kumwondoa mjumbe wa tume ya uchaguzi.

Waziri Mhagama alisema kuongezwa kwa wigo wa msimamizi wa uchaguzi, serikali na kamati, wameridhiana kuweka cheo na sifa lakini pia wameamua kuchukua jina lenye ujumuishi.

"Kwamba mtu ambaye ana sifa za uandamizi, mtumishi mwandamizi kwenye serikali ana uwezo wa kufanya kazi hiyo vizuri. Na katika sifa hiyo, tunao watumishi waandamizi ambao wametekeleza majukumu mazuri tu kwenye tume na mahakama; na maeneo mengine wana uwezo wa kufanya kazi hiyo," alisema.

Mambo mengine ambayo serikali iliyokubaliana na wabunge kutokana na kuwa na mjadala mzito, ni hoja ya kuunganisha jina la Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge, Madiwani na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vitongoji na Vijiji.

Katika Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023, Waziri Mhagama alisema utaunganisha sheria mbili, ambazo ni Sheria Namba 343 iliyokuwa inatumika kwenye uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani na Sheria Namba 292 iliyokuwa inatumika kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa.

Pamoja na mambo mengine, katika majibu yake, Mhagama alisema serikali imeamua eneo hilo nalo lifanyiwe kazi ya kutosha. Alisema serikali imepokea kilio cha wabunge wanawake na wanaume kuhusu suala la jinsia na hasa unyanyasaji wa kijinsia.

"Tunatakiwa kutengeneza mfumo wa kudumu utakaosaidia kudhibiti unyanyasaji wa kijinsia kwa wanaume na wanawake na kufanya mawanda ya uchaguzi kuwa haki, kutoa fursa na kuhakikisha kwamba makosa yanatokana na uchaguzi yanayoweza kupelekea unyanyasaji kuendelea yaweze kukomeshwa," alisema.

Mbali na masuala ya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia kuingizwa kwenye Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Waziri Mhagama alisema serikali imeshaamua kuiwasilisha bungeni, sheria ambayo itasimamia masuala yote yanayohusu unyanyasaji wa kijinsia mahali kote nchini.

"Iwe kwenye uchaguzi, iwe kwenye ndoa, na kila eneo litakuwa na kifungu chake cha kusimamia jambo hili. Kazi hii imefika mahali pazuri.

"Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, imeshapeleka muswada huo kwenye Timu ya Wataalam (IMTC) na sasa tunasubiri waweze kuisogeza sheria hiyo, na Bunge lako tukufu utakapofika muda, tungependa jambo hili lifanyike kabla ya uchaguzi mkuu (ujao) ili kutengeneza mazingira hayo sawa.," alibainisha.

### VYAMA VYA SIASA

Mhagama Alisema wameamua kuchokoza kwa kuja na sheria hiyo ili Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, ianze kutizama kwa jicho la kijinsia, ndani ya vyama vya siasa.

# Mjamzito ajifungua darajani, mafuriko yasomba kichanga

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

UBOVU wa barabara katika Kata ya Bunambiu, wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga, umesababisha mjamzito kujifungua darajani na mtoto wake kusombwa na mafuriko.

Diwani wa Viti Maalum katika Kata hiyo, Hellen Baraza, aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu cha robo ya pili wakati akiwasilisha taarifa ya kata na changamoto zinazoikabili.

Alisema tukio hilo lilitokea hivi karibuni wakati mjamzito huyo ambaye ni mkazi wa kata yake, akipelekwa kwenye kituo cha afya kujifungua baada ya kupata uchungu.

Baraza alisema akiwa kwenye eneo hilo, alishuhudia mjamzito huyo akijifungua salama darajani hapo.

Hellen alisema baada ya kujifungua mtoto huyo akiwa hai kwa kukosa msaada, alisombwa na mafuriko yaliyosababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha wilayani hapa.

Alisema jitihada za watu waliokuwepo kwenye eneo hilo kumtafuta mtoto huyo zilifanikiwa lakini alikutwa akiwa ameshafariki.

Alisisitiza kuwa chanzo cha mjamzito huyo kujifungulia darajani hapo, mtoto kusombwa na mafuriko na kufariki ni ubovu wa barabara.

"Kama barabara hii isingekuwa mbovu, mjamzito yule angewahishwa kwenye kituo cha afya au hospitalini na kujifungua mtoto wake salama," alisema diwani huyo.

Akijibu malalamiko ya diwani huyo na wengine waliowasilisha kero za ubovu wa barabara na madaraja kwenye kata zao katika kikao hicho, Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) wa halmashauri hiyo, Hussein Shaweji, alisema kwa sasa wako katika harakati za ukarabati wa barabara hizo.

Shaweji alisema katika utekelezaji huo, mkandarasi ameshaanza ujenzi wa madaraja, lakini kwa sasa amesitisha kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

HABARI KITAIFA

# Mwili aliyedaiwa kutekwa wakutwa ufukweni

**Na Halfan Chusi**

MWILI wa mkazi wa Magomeni, Dar es Salaam, Mohamed Ameir (35), anayedaiwa kutekwa hivi karibuni na watu wasiojulikana, umekutwa kwenye ufukwe wa bahari eneo la Kigamboni.

Kutokana na tukio hilo, Jeshi la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za mauaji ya mtu huyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, ilieleza kuwa awali jeshi lilipokea taarifa ya kutoonekana kwa mtu huyo Januari 28, mwaka huu.

Kamanda Muliro alisema ndugu wa marehemu walikuwa wanadai ndugu yao alikuwa ametekwa na watu waliokuwa wanataka kupewa Sh. milioni tatu ili kumwachia.

Taarifa hiyo ilisema Jeshi la Polisi bado linaendelea na upelelezi na mahojiano ya kina dhidi ya watuhumiwa waliokamatwa na jitihada zinafanyika ili kuwatia mbaroni wengine walioshukiwa kuhusika na mauaji hayo.

Hivi karibuni kumekuwa yakiripotiwa matukio ya watu kupotea katika mazingira ya kutatanisha, huku ndugu wa jamaa hao wakitoa taarifa katika vituo mbalimbali vya polisi.

Vilevile, kumekuwapo na matukio ya watu kudaiwa kutekwa na watu wasiojulikana na baadaye kupatikana.

Oktoba 10, 2018 mfanyabiashara na muwekezaji wa Klabu ya Simba, Mohamed Dewji aliwahi kutekwa na watu wasiojulikana na kisha baadaye akapatikana.

Vilevile msanii wa nyimbo za kizazi kipya, Roma Mkatoliki, alitekwa April 7, 2017 na watu wasiojulikana kisha baadaye akapatikana.

Pia mmiliki wa mabasi ya Super Sami, Samson Josiah, alitekwa na watu wasiojulikana na baadaye mwili wake ulikutwa ukiwa umetelekezwa katika Mto Rubana unaotenganisha Wilaya za Busega mkoani Simiyu na Bunda mkoani Mara.



Wakazi wa kijiji cha Nguruma, wilayani Arumeru, mkoani Arusha, wakiangalia baadhi ya mizoga ya kondoo wanaodaiwa kuuawa na mnyama anayedhaniwa kuwa ni Chui, kijijini hapo mapema wiki hii. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Mbaroni madai kupandisha bei sukari

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

WAFANYABIASHARA 28 wilayani Tunduru mkoani Ruvuma wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kuuza sukari kwa bei ya juu.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kuhusu tukio hilo, Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, alisema wafanyabiashara hao wamekamatwa baada ya kufanyika kwa msako siku chache tangu serikali ilipotoa mwongozo wa bei ya bidhaa hiyo nchini.

Mtatiro alisema wafanyabiashara hao walikamatwa baada ya kuripotiwa na wananchi wakiuza zaidi ya bei elekezi.

"Baada ya tukio hilo wafanyabiashara hao wamechukuliwa kwenda kutoa maelezo polisi na baadaye kuachiwa kwa dhamana," alisema.

Mtatiro alisema hatua hiyo imefikiwa baada ya kutoa mawasiliano kwa wananchi na kuwataka watoe taarifa kwa mamlaka pale wanapobaini wauzaji wanaokiuka bei elekezi.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara wote wanaouza sukari kuweka vibao vinavyoonesha bei halali kulingana na maelekezo ya bei zikizotolewa na serikali.

Tangu serikali itangaze bei elekezi ya sukari nchini, wadau wengi wamekuwa wakilalamika kuwa agizo hilo halifuatwi na hivyo kutoa wito kwa mamlaka kuchukua hatua

Wakizungumzia tukio hilo, baadhi ya wafanyabiashara wamelalamikia operesheni hiyo wakisema haiwatendei haki kwa kuwa wanauza bidhaa hiyo kulingana na bei wanayonunulia na wakiuza kwa bei elekezi watapata hasara.

"Sisi tulinunua bidhaa hiyo kwa bei zilizokuwa sokoni wakati huo. Sasa tunaambiwa tuuze kwa bei elekezi ambayo haitulipi," alisema mmoja wa wafanyabiashara ambaye hakutaka kutaja jina lake.

Mfanyabiashara mwingine aliyejitambulisha kwa jina la Benjamin, alisema sukari wanayouza walinunua kwa Sh. 3, 600 kwa kilo kwenye maduka ya jumla, hivyo ni lazima wauze bei nzuri ili wapate faida.

Walisema kilichotakiwa ni serikali kwanza wawadhibiti wafanyabiashara wakubwa wanaouza kwa bei ya jumla.

Nao baadhi ya wananchi waliomba serikali kufanya mapitio ya bidhaa zote kwani zimekuwa zikipanda bei kiholela ikiwa ni pamoja na gharama za usafiri ambazo hupandishwa kwa kisingizio cha kupanda kwa nishati ya mafuta.

Walisema lakini bei ya bidhaa hizo hazishuki pindi serikali ikitangaza kushuka kwa bei za mafuta.

# Mbunge atinga na video ya wananchi kunywa maji machafu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Momba (CCM), Condester Sichalwe ametinga na video fupi (clip) bungeni inayoonesha namna baadhi ya wananchi jimboni kwake wanavyotaabika kupata maji safi na salama na kulazimika kuchota maji machafu.

Hali hiyo ilijitokeza jana bungeni wakati mbunge huyo akiuliza maswali ya nyongeza.

Mbunge huyo alisema: "Kwa masikitiko makubwa niseme Wizara ya Maji Momba imepinga kauli ya Rais ya kumtua mwanamke ndoo kichwani, leo nimekuja na clip (video) naomba uletewe mbele hapo Spika uone kama maji haya wana Momba wanatumia binadamu wa kawaida anafaa kutumia haya maji."

"Mwezi wa sita Spika uliniruhusu kuomba mwongozo kwa Wizara ya Maji na kuahidi kuchimba visima vya dharura hadi leo hakuna hata tone la maji, mradi ambao wizara inasema wa Sh.bilioni 9.5, mwaka jana Aprili waliniondoa bungeni kwenda kukabidhi mradi kwa mkandarasi na wakaahidi kufikia mwaka huu Juni mradi utakuwa umekamilika, leo tunavyoongea wiki moja iliyopita ndiyo tumepatiwa Sh.milioni 500 kati ya Sh.bilioni 9.5 na leo mbele ya Bunge Wizara ya Maji inasema utakamilika Desemba,"alisema.

Alisema kauli hiyo ya Wizara ya Maji akienda kuwaambia wananchi anaonekana tapeli.

"Kati yangu na Wizara ya Maji kina nani ni waongo ninaomba Spika uangalie uwe shahidi na ikikupendeza ioneshe video hii kwa wabunge ili Rais aone Watanzania waliomchagua na mimi mbunge mwanamke,"alisema.

Kutokana na ombi hilo, Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson alimuagiza msaidizi wake kumpatia video hiyo ili aangalie na kumtaka Waziri wa Maji, Jumaa Aweso kuzungumzia suala hilo. Akizungumzia suala hilo, Waziri Aweso alisema katika mkutano wa Bunge walipata hoja ya mbunge huyo na walifika jimboni kuona hali iliyopo na kwa dharura alitoa Sh.bilioni moja ili kutatua hali hiyo.

"Niwaombe wabunge wakati mwingine tunaweza kukatisha tamaa watendaji lakini kazi inafanyika na sisi kama wizara ipo miradi ya kimkakati ya kuhakikisha tunasaidia Jimbo la Momba na sisi hatutakuwa kikwazo kwa wananchi kupata huduma ya maji safi na salama katika kumtua mama ndoo kichwani,"alisema.

Kutokana na maelezo hayo, Spika Tulia alisema: "Wabunge mtakumbuka zilitajwa takwimu kuhusu maji Momba akasimama mbunge akasema takwimu hizo kwake yeye hazina uhalisia na akasimama tena katika Bunge la Bajeti maelezo yakatoka vikachimbwe visima vya dharura kwa kuwa magari yamenunuliwa, yakatoka majibu tena hapa alishatoa Sh.bilioni moja yaani ni ya kuongezea kwenye ile Sh.milioni 500 iliyokuwa imetolewa utekelezaji uendelee."

"Hali ya hao wananchi kwenye video niliyokuletea sio ya kukubalika na kwa hiyo maana yake kwenye ardhi hiyo yapo maji ikienda gari kuchimba wakati miradi mikubwa ikiendelea wachimbiwe hivyo visima," alisema.

Hivyo aliiagiza Wizara ya Maji ihakikishe gari la kuchimba kisima linakwenda jimboni humo kutatua adha ya maji iliyopo wakati wanaendelea na utafiti.




Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule (wa tatu kulia), akisimamia operesheni ya kuondoa mabango yaliyowekwa kinyume na utaratibu katika eneo la Morocco, manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam jana. **PICHA: JENIFER GILLA**

# Hatima mama nyama ya swala Februari 16

**Na Francis Godwin,** IRINGA

HUKUMU ya rufani ya mjane, Maria Ngoda, mkazi wa Isakalilo manispaa ya Iringa, aliyehukumiwa kifungo cha miaka 22 jela kwa kosa la kukutwa na vipande viwili vya nyama ya swala, itatolewa Februari 16, mwaka huu.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Iringa, Elvin Mgeta, alisema hukumu hiyo itatolewa saa 5:00 asubuhi baada ya kusikiliza pande zote mbili za mkata rufani na Jamhuri.

Kesi hiyo ilisikilizwa jana katika Mahakama Kuu mkoani Iringa kwa upande wa mawakili wa mkata rufani kuwasilisha hoja zao.

Katika rufani hiyo inayosimamiwa na Jumuiya ya Wanawake Tanzania (UWT), upande wa Jamhuri uliwasilisha hoja zake ukisisitiza hukumu iliyotolewa awali ilikuwa sahihi.

Katika hukumu hiyo, Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya Iringa, Said Mkasiwe, alimhukumu Ngoda kifungo hicho baada ya kumtia hatiani.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa mkata rufani alikuwa na uelewa, hivyo hakuonyesha kuhitaji uwakilishi wa kisheria mahakamani.

Hata hivyo, hoja hiyo ilipingwa na mawakili wa mrufani kuwa suala la uwakilishi wa kisheria mahakamani ni haki ya msingi lakini pia kwa sababu Ngoda hakuwa na uwezo, Hakimu alipaswa kumsaidia katika kumwombea msaada wa kisheria

Pia upande wa Jamhuri ulidai mkata rufani wakati anatoa utetezi wake, alikiri kukamatwa na nyama hoja ambayo ilipingwa na upande wa wakata rufani kwamba hakutaja nyama ya nini na inaweza kuwa ya ng'ombe au vinginevyo.

Aidha, hoja nyingine iliyoibuliwa ni ya suala la mtaalamu wa kutambua kama nyama ilikuwa ya swala au la, jambo ambalo wajibu rufani walidai aliyebaini nyama hiyo kuwa ni swala ana uzoefu wa kutosha wa utambuzi.

Hata hivyo, upande wa mkata rufani uliwasilisha hoja kwamba ndoo iliyokuwa imehifadhia nyama haikufikishwa mahakamani kama sehemu ya Ushahidi, hoja ambayo upande wa Jamhuri ulipinga wakidai haina mashiko.

Kuhusiana na hoja ya Ngoda kuulizwa ikiwa anajua kusoma na kuandika ili apewe fursa ya kuandika maelezo yake baada ya kukamatwa kwa mujibu wa sheria, ilipingwa na upande wa Jamhuri kwa madai kuwa kitendo cha kutia saini kilionyesha alishirikishwa.

Akizungumza nje ya Mahakama, Mwenyekiti wa Chama Cha Mawakili Tanganyika (TLS) Mkoa wa Iringa, Moses Ambindwile, alisema mwenendo wa kesi umekuwa mzuri na pande zote zimesikilizwa kwa haki, hivyo wanasubiri uamuzi wa Mahakama Kuu kwa tarehe iliyopangwa ya hukumu.

# Magari 'mkweche' marufuku stendi ya Mwenge

**Na Gwamaka Alipipi**

WAKATI wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam wakisubiri kufunguliwa kwa Stendi ya Mabasi Mwenge, uongozi wa Wilaya ya Kinondoni umesema haitaruhusu magari mabovu kuingia katika kituo hicho.

Akizungumza na kituo cha Radio One, Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule, alisema kituo hicho kitakapoanza kitaruhusu kuingia kwa magari yaliyosajiliwa na yenye ubora uliothibitishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA)

"Kwa hiyo tutaruhusu magari yaliyosajiliwa kuingia katika kituo hicho, hatutaruhusu gari lolote liingie, magari ambayo ni bora na yenye uimara, na ni utaratibu wa kawaida hata Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani wanasimamia," alisema

Alisema uongozi wa wilaya ya Kinondoni unatamani kuwe na magari mazuri yanayoingia katika stendi hiyo, si gari linaiongia pale linaanza kumwaga mafuta bali liwe vizuri.

"Tutasimamia ubora wa majengo, biashara na huduma zingine zitakazohitajika. Gari ambalo halitakuwa na sifa hizo yanyooshe tu yaelekee kwingineko yasiingie katika kituo hicho," alisema.

Alisema uongozi unahitaji gari liwe bora na liwe na sifa ya kuwa barabarani sambamba na madereva na makondakta wawe wasafi katika mavazi na lugha.

"Gari tutalikagua, dereva wake yukoje au kondakta wake yukoje kwa sababu kile kituo ni kikubwa na kinapokea wageni kutoka sehemu mbalimbali. Hatutaki kumuona kondakta amevaa suruali iliyochanika au amevaa ovyo au tumuone anatoa lugha ya matusi," alisema.

Alisema uwezo wa kituo hicho ni kuchukua daladala 200 kwa wakati mmoja na kwamba magari binafsi yataruhusiwa kuingia lakini yatachangia kiasi cha fedha.

Mtambule alisema gharama zilizotumika kujenga kituo hicho ni Sh. bilioni mbili, hivyo serikali inatamani kuona gharama hizo zinarudi na faida kupatikana.

"Tunataka kile kituo kilete faida na ajira, hatutaki tukute mashimo na mabwawa ya maji, ni lazima tuitunze," alisema.

Kuhusu gharama za kupangisha, Mtambule alisema ni Sh.29,000 kwa mita ya mraba kwa vyumba cha chini, Sh.15,000 kwa kwa vyumba vya juu.

Alisema tangu kukamilisha kwa vyumba vya biashara maombi ya kupangisha yalifika zaidi ya 7,000 na hivi sasa vyumba vyote vimeshachukuliwa na wafanyabiashara.

# Walia na uhaba wa maji mwezi mzima

**Na Beatrice Moses**

WAKAZI wa mitaa ya Saranga na Ukombozi, Ubungo mkoani Dar es Salaam wamelalamika kukosa huduma ya maji kwa takribani mwezi mmoja.

Wamesema hali hiyo inatishia usalama wa afya zao, hasa kutokana na kuzuka kwa ugonjwa wa kipindupindu katika baadhi ya maeneo.

Akizungumza na Nipashe, mmoja wa wakazi wa mtaa wa Ukombozi, Hellen Shirima, alisema inawapa wakati mgumu kwa kuwa kila wanapofuatilia katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) wanapewa majibu kwamba wanashughulikia tatizo.

"Sisi tupo chini ya DAWASA Kinyerezi Saranga kila tunapofuatilia kwa wahusika kuwa maji hayatoki majibu tunayopewa subirini tunafanyia kazi. Sasa ni mwezi unakatika maji hayatoki, tunachota kwenye visima vya watu waliokinga ya mvua," alisema Shirima.

Baadhi ya wananchi wengine wameeleza kuwa kuna taarifa za kuwapo kwa ugonjwa wa kipindupindu, hivyo wanapata hofu kwa kuwa maji safi na salama yanahitajika katika kudhibiti kusambaa kwa ugonjwa huo.

Walisema kwa sasa wanatumia maji ya visima ambapo wakati huu mvua inaponyesha kuna watu hutiririsha maji kutoka kwenye chemba za vyoo.

Mmoja wa wakazi hao, Apolinary Mramba, alisema katika Mtaa wa Mpalula Msikitini wamekumbwa na tatizo la kukosa maji baada ya kuhamishiwa DAWASA Kinyerezi kutoka Kimara.

"Tulilalamika hadi kumshirikisha Mkuu wa Wilaya ya Ubungo kuhusu suala letu, alilifanyia kazi tukawa tunapata maji japo kwa mgawo wa siku ya Jumanne na Alhamis, lakini sasa ni zaidi ya wiki tatu hatuna maji hali ni mbaya," alisema.

Mramba alisema kuwa jambo linalowaondolea matumaini ni kutopata majibu kutoka kwa wahusika ambao baadhi yao wapo pamoja katika mtandao wa Whatsapp, wanawasilisha malalamiko yao lakini hawapewi majibu ya kueleweka.

Nipashe lilimtafuta Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano DAWASA, Evalasting Lyaro, kuhusu suala hilo ambaye alisema kulikuwa na matengenezo ya bomba.

Lyaro alisema: "Kuna matengenezo ya bomba kubwa lilizolewa na maji, likatengenezwa na kukamilika juzi, kwa hiyo watapata maji kupitia mgawo wa Kinyerezi".

HABARI KITAIFA

# Mkakati nishati safi kupikia waiva



Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga akijibu maswali mbalimbali ya Wabunge wakati wa kipindi cha maswali na majibu katika kikao cha 4, mkutano wa 14, jijini Dodoma jana. **PICHA: WN**

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, amesema serikali inakamilisha uandaaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia ili kuhakikisha asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati safi ifikapo mwaka 2033.

Kapinga alisema hayo jana bungeni jijini Dodoma wakati akijibu swali la Jacqueline Msongozi (Viti Maalum) aliyetaka kufahamu mpango wa serikali wa kuweka ruzuku kwenye nishati ya gesi ili wananchi kumudu kununua.

"Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kutatua vikwazo vinavyokwamisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kupunguza gharama za upatikanaji wa nishati safi, vifaa na majiko sanifu ya kupikia," alisema.

Naibu Waziri alisema ajenda ya nishati safi ya kupikia ni ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na hilo lilitiliwa mkazo katika Mkutano wa 28 wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 28) Dubai.

Alisema katika mkutano huo, Rais Samia alizindua mkakati wa nishati safi ya kupikia kwa wanawake Afrika, hivyo Wizara ya Nishati inalibeba suala hilo kwa uzito mkubwa.

Kuhusu ruzuku kwa mitungi ya gesi ili kupunguza gharama ya mitungi hiyo, Naibu Waziri alisema tayari kuna programu na miradi mbalimbali inayoendelea akitolea mfano programu ya ushirikiano na Umoja wa Ulaya (EU).

Katika program hiyo, alisema mawakala wanawezeshwa kifedha ili kupunguza bei ya mitungi ya gesi kwa watu wanaonunua kwa mara ya kwanza na kwamba serikali itaendelea kubuni miradi na kutafuta fedha ili wananchi wapate gesi kwa gharama nafuu.

Naibu Waziri aliongeza kuwa serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikibuni na kutekeleza sera na mikakati yenye lengo la kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia pamoja na utunzaji wa mazingira.

Pia alisema serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) imeanza mradi wa kusambaza nishati safi ya kupikia kwenye taasisi mbalimbali zikiwamo magereza, kambi za jeshi, shule za msingi na sekondari na kwamba kazi hiyo ni endelevu kwa kuwa serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuzifikia taasisi nyingi zaidi.

Kapinga alisema jitihada ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2015 inayoielekeza serikali kuchukua hatua madhubuti za kufanikisha matumizi ya nishati na vifaa sahihi vya kupikia.

# Kamati yaagiza viwanda vya sukari kupunguza makali

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

KAMATI ya Kudumu ya Bunge, Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, imeagiza kiwanda cha sukari cha Mkulazi na kiwanda cha sukari cha Mtibwa vilivyopo mkoani Morogoro, kuhakikisha vinavuna miwa, kuzalisha sukari kwa lengo la kuwapunguzia makali ya bei wananchi.

Imesema inatambua kuwepo kwa tatizo la kujaa kwa maji kwenye mashamba ya viwanda hivyo kulikosababishwa na kunyesha kwa mvua nyingi.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Deo Mwanyika, alitoa maagizo hayo na kusema ni kweli viwanda hivyo vimeshindwa kuzalisha sukari kwa sababu ya maji yaliyotokana na mvua zinazoendelea kunyesha kujaa kwenye mashamba, hivyo miwa kushindwa kuvunwa.

"Tumetembelea mashamba na tumeona mvua zimezidi zaidi ya milimita 720 kutoka kwenye milimita 200, tumeona namna ilivyo ni vigumu kukata miwa na magari kuingia shambani kusomba miwa," alisema Mwanyika.

Kamati hiyo ilifanya ziara hiyo kwa lengo la kuangalia na kujiridhisha changamoto zilizochangia kuwepo kwa upungufu na kupanda kwa bei ya sukari hapa nchini.

Mwanyika alisema kutokana na changamoto iliyopo ya upungufu wa sukari na kusababisha bei kupanda ni muhimu viwanda hivyo wakatumia njia mbadala ya kuhakikisha miwa iliyopo shambani inavunwa na kupelekwa kiwandani kwa ajili ya uzalishaji.

Mtendaji Mkuu wa Kampuni Hodhi ya Mkulazi, Selestine Some, alisema wataanza kuuza sukari wiki ijayo ili kupunguza makali ya bidhaa hiyo.

Some alisema kutokana na mahitaji makubwa ya sukari nchini na kusababisha bei ya sukari kuwa juu kwa kuanzia wataingiza sokoni tani 500.

Alisema kiwanda hicho kinauwezo wa kuzalisha tani 50, 000 kwa mwaka kilipanga kuingiza sukari ya awali sokoni tani 21,000 lakini kutokana na changanoto ya hali ya hewa na mvua mpaka sasa kimezalisha tani 500.

Alisema changanoto hiyo ya hali ya hewa imesababisha kushindwa kuvunwa kutokana magari kushindwa kufika shambani.

Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde alisema serikali inatambua tatizo la upungufu wa sukari uliochangiwa na hali ya hewa na mvua zinazoendelea kunyesha na kusababisha viwanda vya sukari kusimamisha uzalishaji.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila la heri Serengeti Girls katika michuano ya dunia

**TIMU** ya Soka ya Taifa ya wasichana wa umri chini ya miaka 17 maarufu Serengeti Girls inatarajia kuteremka ugenini Zambia leo kuvaana na wenyeji katika mechi ya kwanza ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali zijazo za Kombe la Dunia (U-17).

Serengeti Girls itawakaribisha Wazambia hao katika mchezo wa marudiano utakaochezwa Jumamosi ijayo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Kikosi hicho kinashuka kikiwa chini ya Hilda Masanche anayeshirikiana na Mohamed Mrisho pamoja na Juma Kaseja, baada ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kufanya mabadiliko katika benchi la ufundi, limemtoa aliyekuwa Kocha Mkuu, Bakari Shime, kupunguziwa majukumu.

Timu hiyo inaundwa na idadi kubwa ya nyota walioshiriki mashindano ya vijana wa umri chini ya miaka 15 ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-15), yaliyofanyika mwaka jana na baadaye kuibuka mabingwa wa michuano hiyo Afrika, wakitwaa taji hilo Afrika Kusini.

Ni kikosi kinachokwenda kupeperusha bendera ya Tanzania kikiwa na nyota ambao wamepata mazoezi kupitia michezo hiyo ya kimataifa ya CECAFA, hivyo tunatarajia watapambana kusaka matokeo chanya katika mechi hiyo ya kwanza na kurahisisha kazi kuelekea mchezo wa marudiano.

Katika kuhakikisha Serengeti Girls inafikia malengo yake, kuanzia wachezaji na benchi la ufundi wanatakiwa kuingia katika mashindano ya mwaka huu wakiwa na nguvu na mipango mipya, kutoingia uwanjani na historia ya kilichofanyika katika michuano iliyopita.

Tunawakumbusha kufahamu mashindano yale ambayo Serengeti Girls ilifanikiwa kushiriki nchini India na kutolewa katika hatua ya robo fainali yalimalizika, sasa tunaanza ukurasa mpya.

Wachezaji na benchi la ufundi linatakiwa kujipanga na kuwaheshimu wapinzani ili kuhakikisha tunaanza kwa kupata matokeo chanya, wasiingie uwanjani wakiamini wao ni bora kwa sababu walifanya vyema katika michuano iliyotangulia, wakumbuke Zambia ni moja ya nchi zenye wachezaji wenye vipaji kutoka Ukanda wa Afrika ya Kusini, hivyo hawatakuwa legelege.

Serengeti Girls inatakiwa kuichukulia mechi ya leo kama fainali, kuhakikisha inamaliza kazi ugenini na kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele itakapowakaribisha wapinzani wao hapa nyumbani.

Wawakilishi wetu wanatakiwa kuongeza umakini na kutobweteka katika dakika 90 za ugenini na dakika nyingine kama hizo zilizobakia watakazokuwa nyumbani, mpira ni mchezo wa makosa, utulivu na umakini ndio jambo kubwa litakalowasaidia kupata matokeo mazuri na hatimaye kusonga mbele.

Mbali na kuwakumbusha kujituma wakati wote, tunapenda kuwatakiwa mchezo mwema Serengeti Girls ambayo pia inaundwa na nyota wa Twiga Stars yenye kibarua cha kwenda kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wanawake (WAFCON 2024), zitakazochezwa Juni, mwaka huu huko Morocco.

Ili kufikia malengo, huu ndio wakati mzuri kwa taasisi na makampuni mbalimbali kujitokeza kuidhamini na kuipatia misaada Serengeti Girls, hongera kwa TECNO ambayo jana ilikabidhi jozi za viatu seti 300 kwa ajili ya kikosi hicho, udhamini wa aina yoyote huwaongezea nguvu wachezaji na kujiona wana 'deni' kwa Watanzania.


Tunaamini mashabiki na wadau wengine wa soka pia wataungana na TFF pamoja na serikali kujitokeza kuishangilia timu hiyo itakapowaalika Wazambia, kwa sababu uwepo wao kwa wingi uwanjani hukamilika namba ya mchezaji wa 12.

Tunapenda pia kuitakia mchezo mwema Timu ya Soka ya Taifa ya Futsal ambayo leo inateremka ugenini kwenye Uwanja wa Windhoek Showground nchini Namibia kukutana na wenyeji huku marudiano yakifanyika hapa nyumbani baada ya wiki moja.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wachambuzi msigeuke watabiri, mchezaji hapimwi mchezo mmoja

Na Adam Fungamwango

**HIVI** karibuni kumezuka tabia ya baadhi ya wachambuzi kujigeuza wao ni watabiri.

Mtabiri ni yule anayetabiri kitu ambacho kitatokea huko mbele, kiwe kizuri au kibaya.

Anaweza kutabiri mtu fulani ambaye ni maarufu atafanya hivi, au katika nchi fulani kutatokea mafuriko, moto, neema ya chakula, nzige au vingine vinavyofanana na hivyo.

Kifupi hutabiri amani, majanga na neema kwa nchi, lakini hutabiri watu pia na nini kitawatokea. Kuna wanaotabiri mpaka vifo vya mastaa au viongozi wakubwa.

Sitaki kwenda huko sana, lakini nilitaka kwanza watu wafahamu mtabiri ni mtu wa aina gani.

Mchambuzi wa michezo au soka yeye huchambua kitu ambacho kimeshatokea na anakiangalia kutokana na mawazo, mtazamo kwa jinsi alivyokiona. Na siyo kila mmoja anaweza kuchambua chochote.

Tukija kwenye michezo sasa, hasa mpira wa miguu, kuna wachambuzi wengi wazuri na wakifanya hivyo utapenda na wakati mwingine kufanya mchezo wa mpira wa miguu upendwe.

Kusema kweli huenda kwa sasa Tanzania kuna mashabiki wengi sana wa mpira wa miguu kuliko nchini nyingi za Afrika.

Ni tofauti na miaka ya 1980 hadi 1990, ambapo mpira wa miguu ulionekana ni mchezo unaopendwa na wa watu fulani hivi, wababe, wahuni na wasiokuwa na kazi ya kufanya.

Hata ukienda uwanjani unakutaka na watu wale wale tu. Ukibahatika kuonyeshwa kwenye televisheni na watu wachache tu wanaonekana kutazama.

Kwa sasa mpira wa miguu umekuwa ni kama mchezo wa watu wote, rika zote, wazee, vijana watoto, tena wanaume na wanawake. Majumbani utakuwa hata akinamama wanaangalia soka kama wanavyoangalia tamthilia, kwenye vibanda umiza, unatazamwa na mabishano ya hali ya juu. Uwanjani unakutana na sura tofauti, wake kwa waume na watoto wao pia. Mpira sasa umekuwa kama mtoko wa familia.

Hii yote, pamoja na mambo mengine, lakini wachambuzi wamechagia zaidi mchezo huu kupendwa sana.

Hata hivyo siku za karibuni kumezuka baadhi ya wachezaji ambao kazi yao si kuchambua ila ni utabiri.

Mchambuzi anamponda mchezaji waziwazi na kumhukumu kwa mechi moja tu.

Mfano mdogo, dirisha la usajili limefungwa Januari 15, mwaka huu na kila timu imesajili wachezaji ambao inaona watawafaa kuongeza nguvu kwenye kikosi chao.

Wengine wamecheza mechi moja tu, mbili, wengine hawajacheza kabisa. Lakini wanatokea baadhi ya wachambuzi wanasema kabisa kuwa ni wachezaji wasio na viwango.

Cha ajabu wachezaji wanaohukumiwa wanatoka kwenye klabu zingine kubwa Afrika. Wapo wachezaji ambao walikuwa wanazichezea klabu za humu huku ndani na wamesajiliwa na klabu zingine, kila mmoja akijua uwezo wao.

Lakini kwa sababu ameingia katika klabu nyingine, anaonekana eti hamna kitu.

Mimi nadhani kwa sasa wachezaji waliosajiliwa kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili wanaweza kuhukumiwa mwishoni mwa msimu.

Hapa sasa unakuwa si utabiri bali ni rekodi, takwimu na tathmini ndiyo itakayokuwa imefanya kazi na si kudhani.

Mechi moja, mbili au tatu haiwezi kuwa ya kumhukumu mchezaji aliye kwenye kikosi kipya ambapo anahitaji muda wa kuzoea mazingira, kuzoeana na wenzake, pamoja na mfumo wa timu.

Na hata kama ni mechi moja, mchambuzi anachotakiwa kufanya ni kuchambua zile dakika 90 alizocheza ni kitu gani alichokifanya tu na si baada ya hapo kusema huyu ni kiboko sana au hamna kitu.

Wapo wachezaji wengi waliokuja nchini wakapondwa kwa kuangalia kwa mechi chache, lakini baadaye wakawaumbua.

Hata Emmanuel Okwi na Clatous Chama walipojiunga na Simba kwa misimu tofauti walikuja kama wachezaji wa kawaida tu na usajili wao wala haukuwa wa kutikisa vyombo vya habari na hata michezo yao ya mwanzo haikuwa ya kuvutia. Lakini lao sina haja ya kuongeza kitu walichokifanya ndani ya klabu ya Simba kiasi cha kuacha alama isiyofutika hadi leo.

Fiston Mayele alijiunga Yanga ukionekana ni usajili wa kawaida dhidi ya Heritier Makambo ambaye alikuwa anarejea tena, na kabla ya hapo aliacha jina kubwa. Hata mechi za kwanza alizocheza Mayele alionekana hana lolote ni mchezaji mjanja mjanja tu, lakini leo hii kila mmoja anamtambulia ni nani.

Narudi kule kule kuwaomba wachambuzi kuwa wajikite zaidi katika kuchambua mechi, na mchezaji mmoja mmoja alichokifanya kwa mechi husika, siyo baada ya hapo kuweka mtazamo wake wa mbele ambapo sasa inakuwa na mapenzi ya mchambuzi badala ya uhalisia.

# Kinana: Watanzania changamkieni fursa za biashara

**Na Joseph Mwendapole**

WATANZANIA wametakiwa kuchangamkia fursa ya maduka yote 2,500 yanayojengwa kwenye Kituo cha Biashara cha East Africa Commercial and Logistic Center (EACLC), Ubungo kinachotarajiwa kuanza Juni, mwaka huu, badala ya kuacha nafasi hizo kwa wageni.

Kukamilika kwa mradi huo kutasababisha ajira 15,000 za moja kwa moja na 65,000 za muda kutokana na mwingiliano mkubwa wa wafanyabiashara wa hapa nchini na wa nchi jirani.

Kinana alisema hayo juzi alipotembelea kituo hicho kuangalia maendeleo ya ujenzi wake ambao kwa sasa umeshafikia asilimia 90.

Alisema baada ya kukamilika kwa kituo hicho, hakutakuwa na sababu yoyote tena kwa wafanyabiashara wa nchi za Afrika Mashariki na Kati kufuata bidhaa China kwa kuwa zote zitakuwa zinapatikana kwenye kituo hicho.

"Mimi ningependa kuona maduka yote 2,500 yaliyoko kwenye kituo hiki yanachukuliwa na Watanzania. tusije kufungua eneo kubwa na muhimu la biashara kama hili badala ya kutunufaisha sisi wakafaidi wageni na sisi tukabaki kuwa watazamaji," alisema Kinana.

Mbali na kusaidia kukuza biashara na viwanda nchini, alisema kituo hicho kitakuwa msaada mkubwa kwenye kuimarisha uhusiano mwema ulioko baina ya Tanzania na China.

Alisema serikali imetoa kipaumbele kwenye uwekezaji wa sekta binafsi na ndiyo sababu imeundwa ofisi maalum ya kuwezesha sekta binafsi (PPP) ili kuwezesha kustawi kwa wawekezaji wa sekta binafsi wakishirikiana na sekta ya umma.

Kwa mujibu wa JKinana, kituo hicho mbali na kuchangia kwa kiwango kikubwa kukua kwa uchumi kupitia kodi mbalimbali, kitasaidia pia kuongeza ajira za moja kwa moja kwa vijana wa Tanzania.

Naye Balozi wa zamani wa China nchini, Liu Qingyou, alisema amefurahi kuona uchumi wa Tanzania unaendelea kukua kwa kasi kwa kuweka mazingira mazuri ya biashara na kuzipita nchi nyingi za Afrika.

Alisema pia amefurahi kuona namna viongozi wa serikali walivyotoa msaada mkubwa kwenye utekelezaji wa mradi huo ambao alisema utasaidia kuimarisha uchumi na uhusiano wa Tanzania na China.

"Huu mradi ni mkubwa na utakuwa msaada kwa nchi za Afrika Mashariki kwasababu kila kitu kitapatikana hapa haapa nchini na wafanyabiashara wengi watachukua bidhaa hapa na utasaidia kuchangamsha uchumi wa Tanzania," alisema

Mkurugenzi wa Kituo hicho, Cath Wang, alisema ujenzi huo ambao unatarajiwa kutumia dola za Marekani milioni 110 unatarajiwa kukamilika Juni mwaka huu.

Alisema hiyo ni fursa nzuri kwa wafanyabiashara mbalimbali nchini na kusema kuwa wanaotaka kujua zaidi kuhusu uwekezaji huo wanaweza kufika kwa ajili ya kupata taarifa mbalimbali.



Ofisa Uchunguzi Mwandamizi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara, Greyson Kisanga akitoa elimu kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Anna Abdallah, kuhusu majukumu ya taasisi hiyo katika kuzuia na kupambana na vitendo vya rushwa, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Sheria nchini, wilayani humo juzi. **PICHA: HAMISI NASRI**

# Kiwango kusoma, kuandika watu wazima chapaa

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imesema kiwango cha watu wazima wanaojua kusoma na kuandika kimeongezeka kwa asilimia 6.3 ndani ya miaka 10.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omar Kipanga, alibainisha hayo jana bungeni wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Taska Mbogo.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali ina mkakati gani kuhakikisha Watanzania wote wanajua kusoma na kuandika.

Akijibu swali hilo, Kipanga alisema kulingana na ripoti iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), kwa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Tanzania imefikia kiwango cha asilimia 83 kutoka 78.1 katika Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012. Kipanga alisema katika kuhakikisha Watanzania wote wanajua kusoma na kuandika, serikali imeendelea kutekeleza afua mbalimbali ikiwamo kuondoa vikwazo vya kupata elimu kama vile kutolewa kwa elimu ya msingi bila malipo, elimu ya lazima sasa kuwa ya miaka 10.

Pia alisema kutekeleza programu zenye lengo la kuwafikia Watanzania waliokosa fursa za elimu kwa mfano elimu ya watu wazima na ujifunzaji endelevu, utekelezaji wa mkakati wa kitaifa wa kisomo pamoja na kutoa fursa kwa wanafunzi walioacha masomo kwa sababu mbalimbali kurudi shuleni.

Pamoja jitihada hizo, alisema serikali imeendelea kuboresha huduma za maktaba nchini katika ngazi za mikoa, wilaya na shule ikiwa ni pamoja na maktaba mtandao ili kuwawezesha Watanzania wengi zaidi katika maeneo mbalimbali kupata huduma ya kujisomea huko waliko. Aidha, alisema serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kwa lengo la kuongeza fursa kwa Watanzania wengi zaidi kujiunga na elimu ya watu wazima.

Akiuliza maswali ya nyongeza, Mbunge wa Viti Maalumu (CCM), Fatuma Toufiq, alihoji mkakati wa serikali wa kuwabaini Watanzania wenye umri wa miaka 35 ambao hawapo kwenye afua za kujua kusoma na kuandika wafikiwe.

"Je, serikali ina mkakati gani kuhakikisha shule za msingi na sekondari zinakuwa na maktaba ili wanafunzi wajisomee?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Kipanga alisema takwimu hizo zinathibitisha kuwapo na watu wasiojua kusoma na kuandika na kupitia mipango ya serikali itawafikiwa Watanzania wasiojua kusoma na kuandika.

Kuhusu maktaba alisema katika miundombinu ya shule inayojengwa kwa sasa lazima kuwa na jengo la maktaba.

## Wakwama kwenda shuleni kisa mvua

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe, Prof. William Mwegoha, amesema utafiti mbalimbali unaofanywa na wanataaluma wa chuo hicho umelenga kuwainua vijana wa Kitanzania kwa kuwapatia mitaji kupitia uchangiaji wa umati.

Prof. Mwegoha alisema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa kongamano la kimataifa linalofadhiliwa na serikali ya Denmark kupitia mpango wa kutumia michango ya umati kuwezesha wajasiriamali wadogo nchini (C4YET ) lililofanyika jijini Arusha.

Alisema utafiti huo katika masuala mbalimbali unalenga kuangalia mbinu mbalimbali, faida kwa mlengwa na mchangiaji ili kuwainua vijana na wajasiriamali wadogo kupitia uchangiaji huo.

"Kwa chuo chetu Mzumbe ni utafiti wenye manufaa makubwa kwa sababu unachangia kwenye dhana ya serikali ya kuhakikisha wajasiriamali wadogo wanawezeshwa mitaji," alisema Prof. Mwegoha.

Alisema kupitia kongamano hilo linalowakutanisha watalaamu kutoka vyuo mbalimbali vikiwemo Mzumbe na Chuo Kikuu cha Copenhagen kutoka Denmark, watafiti watabadilishana matokeo ya utafiti na kupata njia sahihi ya kutekeleza dhana ya uchangiaji wa umati.

Prof. Mwegoha amesema mradi huo ulianza mwaka 2019 na ni wa miaka mitano ambao umewanufaisha vijana wa maeneo yote ya mijini na vijijini.

Naye Mratibu wa Mradi huo, Dk. Nsubili Isaga, kutoka Shule ya Biashara ya Chuo Kikuu Mzumbe, alisema mradi huo umewainua wajasiriamali kutokana na kubuni nyenzo walizotumia za uandishi wa andiko lililowavutia wafadhili kwa ajili ya wanataaluma kusaidia utafiti na hatimaye chuo kushirikisha SIDO kuwakwamua wajasiriamali vijana kwenye mikoa ya Arusha, Mwanza, Dar es Salaam, Morogoro na Mbeya.

Aliongeza kuwa wajasiriamali 187 walipewa mafunzo hayo na 100 kati yao walipata mikopo yenye riba ya asilimia tano tu inayowawezesha kuirejesha kwa wakati na baadaye vijana wengine watafikiwa zaidi ili wajiunge na majukwaa ya biashara mitandaoni.

# Mbunge ataka mfumo bora matibabu watoto

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Kinondoni (CCM), Tarimba Abbas ameishauri serikali kuwa na mfumo mzuri utakaosaidia watoto kwenye matibabu, badala kusubiri utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote.

Akiuliza swali bungeni jana, Tarimba alihoji kauli ya serikali juu ya bima ya afya kwa watoto.

"Tunafahamu kwa miaka yote tunamikakati ya kujenga taifa bora la kesho na ili kufanikisha hilo ni lazima kuhakikisha watoto wanakuwa na afya bora, kwa kutokuwa na mfumo sahihi kwa ajili ya watoto ni kufifisha hali ya taifa kujenga watoto vizuri kiafya," alihoji Tarimba.

Naibu Waziri wa Afya, Dk.Godwin Mollel, alisema kauli ya serikali kuhusu bima hiyo ni kuwaomba Watanzania, viongozi wa kisiasa, kidini na kimila kungana na serikali katika kuhamasisha umma kujiunga na bima ya afya kwa wote pale mchakato utakapoanza.

Aidha, alisema serikali ina mifumo mizuri na hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan alifika Hospitali ya Benjamin Mkapa kuwajulia hali watoto waliokuwa wakiumwa ugonjwa wa selimundu ambao wazazi hawakuwa na uwezo wa kugharamia matibabu ambayo kwa mtoto mmoja ni zaidi ya Sh.milioni 50.

"Watoto wametibiwa bure na mwaka huu watoto zaidi ya 20 watatibiwa, katika taifa hili watoto milioni 1.5 wapo kwenye mfumo wa bima wa sasa na wengine wanatibiwa kwenye mifumo mingine iliyopo nchini," alisema.



Mtaalam Mwandamizi wa Fedha na Meneja wa Programu ya CookFund ya Shirika la Umoja wa Mataifa la mitaji ya maendeleo (UNCDF), Immanuel Muro (kulia), akichangia mada kuhusu sekta ya nishati, wakati wa mkutano wa tano wa ushirikiano wa nishati nchini Tanzania (TECS), uliodhaminiwa na Umoja wa Ulaya (EU), UNCDF, UNDP na USAID, jijini Arusha hivi karibuni. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa Eenovators Ltd, Chris Mboni na Mtafiti na Mhandisi Mwandamizi kutoka Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO), Atupele Kilindu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampuni yatajwa mtandao wenye ubora

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imeitangaza kampuni ya simu ya Tigo kuwa kinara kwa kuwa mtandao wenye ubora zaidi miongoni mwa kampuni zote nchini kwa mwaka 2023.

Katika ripoti ya 2023, robo ya nne iliyotolewa Januari 2024, TCRA ilibainisha Tigo kuwa kinara baada ya kutathmini zaidi ya matukio 280 ya viashiria muhimu vya utendaji kazi (KPI) kwa watoa huduma wote wa mtandao wa simu nchini.

Tigo iliibuka mshindi wa jumla katika viashiria vilivyopimwa kuanzia Oktoba mpaka mwezi Desemba mwaka jana.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Ofisa Mkuu wa Biashara wa Tigo, John Sicilima, alisema mafanikio hayo yametokana na uwekezaji wa kimkakati wa kampuni hiyo katika kuboresha na kupanua mtandao katika kipindi cha miaka miwili iliyopita.

Kampuni hiyo, alisema iliazimia mwaka 2022, kuwekeza zaidi ya Sh. trilioni moja ndani ya miaka mitano ili kuboresha miundombinu ya mtandao wake.

"Hii iliwezesha kuzinduliwa kwa teknolojia ya haraka zaidi ya 5G pamoja na kuboresha tovuti zote hadi teknolojia ya 4G katika mikoa yote Tanzania Bara na Zanzibar. Lazima tukubali uwekezaji huu umeboresha kwa kiasi kikubwa mfumo wetu wa kidijitali na miundo yetu ya mtandao," alisema Sicilima.

Alisema taarifa ya mafanikio hayo ya kuwa mtandao wenye mtandao bora hapa nchini kwa robo ya nne ya mwaka imekuja siku chache baada ya kampuni kupokea tuzo ya hadhi ya juu ya Ookla, Desemba mwaka jana kwa kuwa mtandao wenye kasi zaidi nchini. "Kama kampuni tutaendelea kuboresha shughuli zetu ili kuwapa watanzania huduma bora ya mawasiliano ya simu, tunaishukuru TCRA kwa ripoti yao ambayo niatupa mwanaga wa kuona nini tunatakiwa kufanya," alisema.

# CBE yataja faida kusoma shahada umahiri mtandaoni

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE), kimeanza kutoa shahada za umahiri kwa njia ya mtandao kwa fani sita njia ambayo imeanza kuchangamkiwa na wasomi wengi kutokana na kuwa nafuu kulinganisha na kusoma darasani.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof, Edda Lwoga, alisema juzi juijini Dar es Salaam wakati wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kuanzishwa kwa kozi hizo.

Alisema CBE imekuwa ikitoa shahada za umahiri takribani 10 katika fani za biashara na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano TEHAMA na sasa kimeona ni wakati mwafaka kuanza kufundisha kwa njia ya mtandao.

"Kwa sasa tumeanzisha shahada sita za umahiri mtandaoni kwa fani sita. Tayari tumeanza kupokea maombi kwa muhula wa Machi na kusoma kwa njia ya mtandao (online). Kuna faida kadhaa ambazo zimefanya njia hii ya kujifunza kuwa maarufu na yenye ufanisi kwa watu wengi," alisema

Aidha, Prof. Lwoga alitaja faida za kusoma kwa njia ya mtandao kuwa kunamwezesha mtu kusoma kutoka mahali popote na wakati wowote unaofaa bila kujali eneo lake au muda wa siku.

"Kusoma kwa mtandao mara nyingi hupunguza gharama zinazohusiana na elimu, kama vile usafiri, malazi, na vifaa vingine. Hii inafanya elimu kuwa nafuu zaidi na inawapa watu fursa ya kufuata masomo bila kuhitaji kuhamia au kutenga bajeti kubwa," alisema.

Prof. Lwoga alisema njia hiyo inawapa wasomi uwanda mpana wa kuchagua programu na inaruhusu wanafunzi kuchagua masomo yanayolingana na malengo yao na maslahi yao, bila kujali wanavyoishi.

Alisema kusoma kwa mtandao mara nyingi humuunganisha mwanafunzi na teknolojia za kisasa kama vile majukwaa ya mtandao, mabaraza ya mazungumzo na zana za ushirikiano na inaboresha uzoefu wa kujifunza. Njia hiyo, alisema inamwezesha mwanafunzi kushirikiana na wenzake kutoka sehemu mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Alisema kupitia njia hiyo wanafunzi wanaweza kusoma kwa kasi yao wenyewe, kurudia sehemu zenye changamoto, au kuchunguza zaidi masomo yanayowavutia na kwamba inaruhusu kila mtu kujenga uelewa imara wa mada wanazojifunza.

Pia alisema wanafunzi wa kusoma mtandaoni wanapata uzoefu wa matumizi ya teknolojia, ambayo ni ujuzi muhimu katika ulimwengu wa kisasa wa kazi na inawawezesha kuwa tayari kwa changamoto za teknolojia kazini.



## Mawakili wa kujitegemea wapewa changamoto Singida

**Na Elisante John,** SINGIDA

SERIKALI mkoani hapa, imewataka mawakili na wanasheria wa kujitegemea mkoani hapa kuwasaidia wananchi kupata haki kupitia vyombo vinavyotafsiri sheria nchini.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba alitoa rai hiyo juzi wakati wa kilele cha Siku ya Sheria nchini, iliyofanyika kimkoa kwenye Viwanja vya Mahakama ya Hakimu Mkazi mkoani hapa.

"Leo ni siku muhimu, ikiwa ni kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Sheria, niwaombe wanasheria, msitumie vibaya taaluma yenu kama fimbo na njia mojawapo ya kuwaadhibu wananchi wasiokuwa na uelewa mpana wa kisheria, badala yake wasaidieni kutafsiri ili wasipoteze haki zao," alisema Serukamba.

Aliwataka wananchi kutendeana haki baina yao ili kulirahisishia kazi Jeshi la Polisi kusimamia majukumu yake na kuirahisishia mahakama kutoa haki kutokana na ushirikiano kati ya pande hizo tatu.

Awali, Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Mkoa wa Singida , Alluu Nzowa, alisema kitaifa maadhimiaho hayo yalianza Januari 24-30 mwaka huu jijini Dodoma.

Nzowa, alisema mwaka wa Mahakama 2024 ni kiashirio tosha cha kuanza kwa mwaka mpya wa muhilimili huo nchini na kusisitiza kuwa kwa sasa upo kazini.

Mwakilishi wa Mawakili wa kujitegemea mkoani Singida, Wakili Cosmas Luambano, alisema taasisi zinazotoa haki nchini zinaongoza kulalamika kwamba zinakosa haki.

Kutokana na hali hiyo, Luambano alizitaka mamlaka husika kuhakikisha zinajali na kutoa huduma muhimu, ikiwemo kuboreshewa mazingira ya kazi.

Tangu mwaka 1996, Mahakama ya Tanzania imekuwa ikiadhimisha siku hiyo.

# Wajanja watafuna mamilioni ya TCCIA

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MWENYEKITI wa Chemba ya Wafanyabiashara, wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) Mkoa wa Dodoma, Khamis Fungameza, ameiomba Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kufanya uchunguzi upigaji wa mamilioni ya fedha za mradi wao wa vibanda na maegesho ya magari.

Fungameza alitoa ombi hilo jana jijini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu upigaji wa fedha za mradi huo unaofanywa na baadhi ya watu ambao hakutaja majina yao.

Alisema mradi huo wa vibanda na maegesho ya magari uliopo eneo la Kizota ni mali ya TCCIA Dodoma, lakini kuna watu wamejimilikisha na kukusanya mapato kwa manufaa yao binafsi.

"Mradi huu sisi TCCIA hatupati kitu, Serikali pia inapoteza mapato kwani watu hawa hawalipi kodi ya serikali naviomba vyombo kama TAKUKURU, mkuu wa mkoa watusaidie ili mradi huu urudi kwetu kwani hivi sasa watu wachache ndiyo wananufaika nao," alisema.

Alisema vitabu vya mahesabu vinaonyesha watu hao wamekuwa wakikusanya zaidi ya Shilingi milioni 90 kwa mwaka kwenye vibanda.

"Fedha zote hizi wanagawana bila TCCIA kupata hata shilingi, hivyo tunaomba uchunguzi ufanyike ili sisi tupate haki yetu na serikali mapato yake," alisema.

Alitaja moja ya sababu zinazochangia TCCIA kushindwa kunufaisha wanachama wake kuwa ni viongozi wengi kuwa na maslahi binafsi.

"Pamoja na jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan kuzunguka na Rais wa TCCIA maeneo mbalimbali kusaini mikataba ya uwekezaji, sisi hatuwezi kufanikiwa kutokana na viongozi tulio nao wengi wao hawajaingiakutumikia wanachama wetu bali kwa maslahi yao binafsi.

"Wengi ambao wameingia walikuwa ni watumishi baada ya kustaafu wanakuja kutaka uongozi huku wengine wanakuja huku kuficha biashara zao zenye makandokando, " alisema Fungameza.

Vilevile, alisema umoja kwa wafanyabiashara ndiyo silaha kubwa, lakini wao wamekuwa na migogoro ya muda mrefu ambayo haina tija kwa maendeleo ya sekta hiyo.

"Hivi sasa nchini kwetu mitaji kwa wafanyabiashara imekuwa kilio cha wengi, ukiomba mkopo benki unaupata baada ya miezi hata mitatu, lakini wenzetu nchi kama China unaomba asubuhi mchana unaingia na hakuna masharti magumu kama hapa, hivyo hatuwezi kufanikiwa kabisa kuwa kama wengine," alisema

Hata hivyo, alisema kama wangekuwa na umoja wangefanikiwa kuishawishi serikali kuzungumza na taasisi za fedha nchini ili wapate mikopo ya riba nafuu na kwa muda mfupi.



Mshauri Mkuu wa Rais wa Taasisi ya vijana inayojishughulisha na maswala ya amani na maendeleo ya uchumi (YPDEA), Askofu Vicent Malendo akizungumza kwenye ufunguzi wa kikao cha wanachama kwa ajili ya kujadili maendeleo na uchumi, jijini Dodoma jana.
**PICHA: PETER MKWAVILA**

# Serikali, wadau wa elimu kushirikiana

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeahidi kuendelea kushirikiana na wadau wa elimu kutatua kero zinazowakabili watoto wa kike nchini kufikia ndoto kielimu.

Mkurugenzi wa Elimu Maalum Tanzania, Dk. Magreth Matonya alitoa ahadi hiyo juzi kwenye uzinduzi na makabidhiano miundombinu iliyojengwa na Taasisi ya Flaviana Matata kwa ufadhili wa Taasisi ya Segal Famiy katika Shule ya Sekondari Manyunyu mkoani Njombe.

Miundombinu hiyo ni pamoja na matundu 12 ya vyoo, sehemu ya kunawia mikono, chumba maalumu kwa wanafunzi wenye mahitaji, chumba maalum kwa wasichana kujisitiri na sehemu ya kuchomea taka.

Akizungumza kwenye hafla hiyo kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda, Dk. Matonya alipongeza taasisi hiyo kwa kuunga mkono jitihada za serikali kuboresha mazingira ya elimu ili watoto hao wafikie ndoto zao bila vikwazo.

Mwanzilishi wa Taasisi hiyo, Flaviana Matata alisema kuwa: "Msaada unaotolewa na taasisi hii ni muhimu sana kwa kuwa mahitaji ya usafi wa mazingira kwa wasichana ni mpango ambao si tu unaunda mazingira bora na safi bali unaondoa vikwazo vinavyowazuia kuendelea na elimu yao.

Tunaamini kwa kuendelea kutatua changamoto hizi kutachochea mabadiliko chanya sasa na kwa miaka ijayo."

Alihamasisha jamii na serikali kuboresha upatikanaji wa elimu bora kwa watoto wa kike kwa mazingira ya shule na kufadhili masomo kwa wanaotoka mazingira magumu.

Alisema taasisi yake imekuwa ikitoa elimu ya hedhi salama na afya ya uzazi, ugawaji wa taulo za kike shuleni, vifaa vya kujifunzia na kufundishia na kuwawezesha mabinti waliokatisha masomo kurejea shuleni.

"Mradi huu utanufaisha wanafunzi takribani 910 kila mwaka katika Shule ya Sekondari Manyunyu," alisema.



# Vijana watakiwa kukienzi Chama Cha Mapinduzi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) visiwani hapa, Tunu Juma Kondo, amewataka vijana kukienzi na kukitunza chama hicho kwa vitendo ili kufikia malengo ya kuanzishwa kwake.

Tunu alitoa rai hiyo jana wakati akifungua mafunzo kwa wenyeviti na makatibu wa ngazi za tawi hadi jimbo katika Wilaya ya Kati Unguja, ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya CCM kutimiza miaka 47 ya kuanzishwa kwake.

Alisema lengo la kuadhimisha siku hiyo ni kuwaenzi na kuwakumbuka waasisi wa CCM kutokana na mchango waliotoa wakati wa kupigania Uhuru wa Tanzania.

Aliwataka wanaCCM kusaka wanachama wapya watakaosaidia kukipatia usindi wa kishindo chama hicho katika uchaguzi mkuu utakaofanyika nchini mwakani.

Tunu aliwapongeza viongozi wa UWT wa wilaya hiyo kwa kuandaa mafunzo hayo ambayo yatawasaidia viongozi hao kufanya kazi kwa ufanisi na kuzidi kukipatia ushindi CCM mwaka 2025.

Hata hivyo, aliwataka kutunza siri, kufanya uhakiki katika madaftari na kufanya vikao vya mara kwa mara ili kujadili na kutoa maamuzi yanayofaa na kuwasirikisha viongozi wao wakiwemo wabunge, wawakilishi na madiwani.

Akiwasilisha mada ya udhalilishaji katika mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Siti Abasi Ali aliwataka wanachama wa umoja huo kuwa makini katika malezi na kukemea vitendo vya udhalilishaji miongoni mwao vinavyozidi kuongezeka siku hadi siku na kuathiri jamii.

Katibu wa UWT Wilaya ya Kati, Rehema Kondo, alisema katika shamarashamra za CCM kutimiza miaka 47, wameongeza idadai ya wanachama wapya wasiopungua 3,000 katika Wilaya hiyo.

# Kaya 600 sasa kuuaga umaskini

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

KAYA 600 visiwani hapa zinatarajia kunufaika na mafunzo yanayofadhiliwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ya jinsi ya kuondokana na umaskini wa kipato kwa kujiajiri kwa ufundi na upishi.

Desemba mwaka jana TEA ilizindua mpango wa ufadhili wa mafunzo hayo kwa vijana wa kaya maskini na wanaoishi mazingira magumu kwa Zanzibar.

Mafunzo hayo ya muda mfupi yalikuwa yakitolewa kati ya wiki mbili hadi miezi mitatu kwa vijana kutoka kaya maskini waliosajiliwa katika Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ili waweze kujikomboa kiuchumi na umasikini.

Mpango huo umewawezesha vijana hao 300 wa Kisiwa cha Unguja na wengine 300 Pemba kupata ujuzi wa mapishi, kilimo cha mbogamboga, ushonaji, ufundi magari, umeme, bomba na uchomeleaji vyuma.

Akizungumza juzi katika hafla ya kuwapongeza na kuwatunukia vyeti wanufaika hao iliyofanyika Kaskazini Unguja, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Mwanakhamis Ameir, alisema ni wakati mwafaka kwao kuingia mitaani kusaka fursa kwa kutumia ujuzi na vyeti vyao.

"Ni wakati wa kwenda kujichangaya mtaani ili fursa ziwaone maana zipo kila mahali ila sharti ni lazima utoke hapo ulipo, ufanye kitu hata kama kitakuwa hakikulipi kwa wakati huo ili ujuzi ulio nao uonekane na mwisho fursa zitakufuata, alisema.

Aliipongeza Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kutambua kaya masikini katika jamii na changamoto zinazozikabili ikiwemo kipato duni.

Alisema serikali hizo kupitia Mradi wa Kuendeleza Ujuzi (SDF) zilibaini njia mbadala ya kupunguza makali ya ugumu wa maisha kwa kaya hizo ni kuwapatia ujuzi vijana wao.

"Mradi huu unaendana na vipaumbele vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuandaa mageuzi katika sekta ya elimu kwa kuwekeza katika mafunzo ya amali," alisema Dk. Mwanakhamis. Akisoma taarifa ya utekelezaji wa mradi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Bakari Silima, aliishukuru TEA kwa kuwapa ufadhili vijana hao kutoka kaya maskini ili waondokane na umaskini.

Dk. Silima, alisema kutokana na kipato duni, vijana hao wanakwama kufikia fursa, hivyo wamekuwa wakiwahimiza kujiunga katika vikundi wapate msaada kutoka kwa mashirika, taasisi na Serikali kupitia vyama ushirika. Mwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Ephrahim Simbeye, alisema mwaka 2020/2021, Serikali na Benki ya Dunia (WB) zilikubaliana kuanzisha ufadhili wa mafunzo hayo kwa vijana kutoka kaya maskini.

Kaimu Mkurugenzi Utafutaji Rasilimali na Usimamizi wa Miradi wa TEA, Masozi Nyirenda, alisema lengo lilikuwa kufadhili mafunzo kwa wanufaika 4,000 nchini. Nyirenda, alisema wamevuka lengo kwa kuwanufaisha vijana 4,063, wakiwemo hao 600 wa Zanzibar.




Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Mwanakhamis Ameir (wa tatu kushoto), akikabidhi cheti kwa mmoja wa wanufaika wa mpango wa ufadhili kutoka Kaya maskini waliosoma mafunzo ya amali kupitia ufadhili wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), katika mahafali yaliyofanyika Mkokotoni, Unguja jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ufundishaji kichina wapamba moto

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhamed Mussa amesema Serikali ya Zanzibar inathamini mchango wa Taasisi ya Vijana ya Sino-Africa (SAY) kuendeleza sekta ya elimu visiwani hapa.

Mussa aliyasema hayo kwenye hafla ya uzinduzi wa muhula mpya wa kituo cha kujitolea iliyofanyika Tomondo Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja jana.

Alisema kupitia mradi wa elimu ya Kichina wa Zanzibar kumekuwa na mafanikio makubwa ya msingi kwa SAY kwa miaka iliyopita hasa kuendeleza lugha hiyo.

Alisema mradi huo hautoi fursa kwa wanafunzi wa Zanzibar pekee kujifunza Kichina, bali unaweka msingi imara kwa maendeleo ya muda mrefu ya elimu ya lugha hiyo kupitia mafunzo ya walimu na hatua nyingine za kuunga mkono.

Alisema ushirikiano na SAY unaweza kutoa wanafunzi rasilimali tajiri za elimu na kuimarisha ubora wa ufundishaji wa Kichina.

"Natumai msingi wa SAY utasaidia skuli za Zanzibar kupata upatikanaji wa kawaida wa programu za bure za chakula cha mchana kwa wanafunzi," alisema.

Alisema mpango huo wa chakula cha mchana ni muhimu kwa kukuza hamasa ya wanafunzi kujifunza, ustawi wao kimwili na kiafya.

Alisema programu hiyo inaweza kuzingatia maendeleo ya wanafunzi na kuwapa mazingira bora ya kujifunzia.

Aliishukuru timu ya matibabu ya Kichina kwa kusaidia shule na wanafunzi wa Zanzibar kupitia miradi ya SAY.

Mkuu wa Timu ya Madaktari wa Kichina, Jiang Gooqing, alisema anaelewa mapenzi Serikali ya China na wananchi wake wanayo kwa Wazanzibar ya dhati kwa kutoa msaada unapohitajika.

"Mwaka huu ni kumbukumbu ya miaka 60 ya kuwepo kwa timu za madaktari wa China visiwani Zanzibar, hatua muhimu na imekuwa ikifanya kazi kwa miezi minne na kuwasaidia wagonjwa wengi," alisema.

Alisema wapo tayari kuwasaidia wanafunzi maskini kupata mazingira bora ya kujifunzia na kwamba timu hiyo ya madaktari imejitolea kutoa mchango kugharamia chakula cha mchana kwa wanafunzi wengine.

Shule za Kiponda, Hasnuu-Makame, Jendele, Tumbatu, Regeza-Mwendo, Dunga, Chwaka na Makoba, zimeanzisha mafunzo ya Kichina kwa wanafunzi wake.



NICK MINAJ UK. 14



Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



# WAPI HUKO? Atakayelia ndiye mwenyewe

RAPA mwenye nyimbo zenye utata nchini,Emmanuel Elibarick maarufu Nay wa Mitego, anaendelea kupata shinikizo kutoka kwa wananchi wa Kenya, wakidai hata akijikosha vipi wimbo wake mpya unaisema nchi yao.

Nay wa Mitego ametambulisha wimbo wake unaoitwa 'Wapi Huko' na kuzusha sintofahamu baada ya rais wa nchi hiyo jirani kuonekana kukasirishwa wakidai wimbo huo unawagusa wao.

Wimbo huo ambao unafanana na kitabu cha Kusadikika cha mwandishi mashuhuri nchini Shaban Robart, unaelezea nchi moja ambayo ina neema lakini hakuna usawa, ufisadi na uongozi unaoyumba.

Hata hivyo, katika taarifa yake rapa huyo amekanusha wimbo huo kuigusa nchi hiyo na kueleza hakutaja taifa lolote na hivyo hakuna haja ya kutaharuki.

"Wimbo wangu mpya 'Wapi-Huko' sijataja jina la nchi lakini jirani zetu Kenya naona wameamua kuuchukua huu wimbo na kusema ni wao. Yaani nimewaimbia wao kufuatana na hali ya maisha ya nchi yao" amesema Nay wa Mitego kupitia ukurasa wake wa Instagram.

Hata hivyo, vyombo vya habari nchini humo vimeendelea kuuchambua wimbo huo na kueleza msanii huyo hana haja ya kukana kwani kila kitu alichokisema kinawagusa.

Wanaeleza katika nchi za Afrika Mashariki Kenya pekee ndio ina vijana wengi waliosoma ambao wametajwa ndani ya wimbo huo kuwa kuzungumza Kiingereza kizuri na kujigamba jinsi nchi yao ilivyo bora kuliko majirani zao, lakini nyumbani kwao hawana hata umeme.

Hata kuhusu uongozi kulalamika na kujilimbikizia mali wanadai unaendana na hali halisi ya nchi hiyo, hivyo ni vyema kwa msanii huyo kuweka wazi kwamba wimbo huo unaisema Kenya.

BASI SAWA

## Founder Tz akimbiza ngoma mpya

MWANAMUZIKI anayekuja kwa kasi Founder Tz, amewakimbiza wasanii wakubwa wa Bongo Fleva nchini baada ya kibao chake kipya 'Niepushie' kufanya vizuri katika majukwaa ya muziki.



Ngoma hiyo iliyotoka siku tano zilizopita, imepata watazamaji zaidi ya 280,000 na kuwapeleka mchakamchaka masanii maarufu Harmonize, ambaye kibao chake Made It kinaongoza kwa kuangaliwa na watu wengi.

Wimbo huo wa Founder Tz unaelezea namna msanii huyo anavyoamini Mungu pekee ndiye anayeweza kumuepusha na mabalaa pamoja na kumuonyeshea njia ya kufika mbali kimuziki.

## Malha kutoka Comoro atambulisha 'Wako'

MWANAMUZIKI kutoka Comoro, Malha ambaye ameachia ngoma yake mpya 'Wako', amesema mazingira ya Tanzania yanafanana na nchi yake ikiwamo lugha na muziki.

Malha ambaye yuko nchini katika ziara ya kutangaza wimbo wake huo ameeleza kwamba anafurahia kuona ukarimu wa Watanzania kiasi ambacho hawezi kujutia kuja nchini kutambulisha ngoma yake hiyo mpya.

"Wacomoro wako sawa na hapa Tanzania na hata lugha yetu iko sawa na Kiswahili na ndio maana nimeona nije hapa kutambulisha wimbo wangu mpya 'Wako' kwa mashabiki wa muziki ambao naamini wataniunga mkono," amesema Malha.






## HARMONIZE NOMA KWENYE 'MADE IT'

NGOMA mpya ya mwanamuziki wa Bongo Fleva, Harmonize 'Made It' akiwashirikisha wasanii wa nje Mmarekani Bobby Shmurda na Bien Aime Baraza kutoka Kenya, ameonyesha umahiri wake wa kuimba kwa lugha ya Kiingereza.

Msanii huyo ambaye anamiliki lebo ya Konde Music Worldwide, amekuwa miongoni mwa wasanii wachache ambao wamefanikiwa kuimba kwa lugha hiyo na kujipatia umaarufu katika bara la Afrika.

"Maisha ni kitu cha ajabu sana, sikuweza kwenda shule hata kidogo, lakini sasa hivi (Kiingereza) ni lugha yangu," amesikika Harmonize akisema baada ya kuachia ngoma hiyo kwa mara ya kwanza.





## Dulla Makabila msikilize Majizo

MASHABIKI wa mwanamuziki wa singeli, Dulla Makabila, wameonekana kuwa na furaha kutokana na mmiliki wa kituo cha radio cha EFM, Majizo kumuunga mkono msanii huyo katika sakata lake na Haji Manara.

Juzi Majizo alimpatia nasaha nzito Makabila akimwambia

baada ya siasa jambo gumu linalofuatia ni mapenzi, akimuonya kwamba lazima aelewe na kutambua ugumu wake kutokana na viumbe kuishi kwa utashi na kubadilika badilika bila kujua kwa nini.

Baadhi ya watu ambao wengi wao ni wafuasi wa Makabila walishiriki maoni katika ujumbe huo na kuonyesha furaha yao kwamba yuko upande wa Dulla Makabila, licha ya ujumbe huo kuonyesha unazunguka na kutotaja mlengwa.

## ABDALLAH SI NDIYO DULLA?

**Na Adam Fungamwango**

MAMBO yamekuwa mengi sana mwezi Januari hadi muda umekuwa mchache. Mwezi umemalizika kwa matashtiti, patashika nguo kuchanika.

Mipasho si mipasho, ili mradi tu tafrani tu moja kwa moja.

Na hii ni baada ya msanii wa singeli Dulla Makabila kutoa ngoma yake aliyoiita 'Furaha.'

Wale wadadisi wa mambo wakasema wakadai kuwa ngoma hiyo amemuimba mtalaka wake.

Sitaki kwenda mbali sana kwenye hili, lakini baada ya wimbo huo ulipigwa kwa mtindo wa singeli, wasanii wengine nao wakadandia hoja, nao wakatoa ngoma zao na kuufanya mwezi Januari nao uzalishe ngoma kadhaa za mtindo huo.

Tulitoa ngoma 10 za bongo fleva ambazo zilizofunga mwaka 2023 ambazo zilifyatuliwa mwezi Desemba. Kama vile haitoshi tukaja na pini 10 ambazo zilitoka mara tu baada ya mwaka 2024 kuingia.

Lakini kumbe mwezi huu kutokana na sakata la Dulla Makabila umezalisha ngoma kadhaa za singeli. Hebu tusicheki hizi tano ikiwemo ya yake mwenyewe.

**Furahi-Dulla Makabila**

Bado mpaka sasa inatikisa. Imeshika namba moja katibu mwezi mzima kwenye mtandao ya 'you tube' na sasa imeshuka nafasi moja, ipo namba mbili.

Ngoma ilipandishwa Januari 19 na maudhui yaliyomo kwenye pini hii ndiyo imesababisha mwezi Januari kuwa wa moto. Wapambe na machawa wakidai Dulla kamuimbia mkewe wa zamani. Wasanii wengine wakadandia na kuona ndiyo hapa hapa.

**Yatamkuta-Meddy PHD**

Goma moja kati la singeli lilitolea Januari 21, siku mbili tu baada ya Dulla kufyatua wa kwake.

Meddy PHD katika ngoma hii aliyoiita 'Yatamkuta' ni kama anambebeleza rafiki yake akiwambia asihuzunike sana na kama kuna lolote baya amefanyiwa, basi waliyomfanyia nao yatawakuta.

**Abdallah si ndiyo Dulla?-Duoz**

Siku moja tu baada ya Meddy PHD kutoa ngoma yake ya singeli, yaani Januari 23, msanii mwingine Duoz akaona wala isiwe tabu, akishirikiana mwenzake Yublavah, wakaingia studio na kurekodi ngoma ambao wenyewe wakaiita 'Abdallah si ndiyo Dulla?'

Maudhui ya wimbo huu yako katikati, kuna eneo wanamuonea huruma jamaa yao, na wakati mwingine wanamponda, kisa mapenzi yanampeleka lesi.

**Bado Hujasema-Meja Kunta**



Menja Kunta yeye amekuja kivyake. Wala hakugusia chochote kuhusu suala la Dulla. katoa ngoma yake Janauari 25 akaiita 'Bado Hujasema.'

Kuna msichana anayempenda, lakini anamsumbua. Mara aseme pua lake baya, mara ana bichwa kubwa, mara ana sura mbaya, halafu ana domo kubwa. Sasa jamaa kaamua kwenda kwa mganga wa kienyeji ili amfanyie mambo fulani binti yule ili amuone mzuri, 'hendisamu.'

**Madimbeni- DJ Hajiz Jini**

'Madibeni,' ni ngoma iliyopandishwa kwenye mtandao wa kijamii Januari 28 na msanii DJ Hajiz Jini.

Ni moja kati ya ngoma mpya za singeli zilizotoka mwanzoni mwa mwaka huu 2024 na kuzoa mashabiki wengi uswazi.

FILAMU

## Watoto wa mitaani: Mazoea yana tabu

**Na Adam Fungamwango**

MAZOEA siku zote yana tabu. Haijalishi umezoea tabu au raha. Wapo watu ambao wamezoea kukaa kijijini, wanapofika mijini na kukaa wiki moja tu hamu inawaishia wanataka kurudi walikotoka. Ni kwa sababu ya mazoea.

Kuna wanaotoka mjini kwenda kijijini, nao wanapokutana na mazingira ya huko, yanawashinda kutokana na kuzoea kuishi mjini, hivyo wanashindwa.

Hata leo hii mkazi wa 'uswazi', anaweza kushindwa kukaa 'ushuani.'

Tunaitazama filamu ya 'Watoto wa Mitaani', imechezwa na wasanii wengi chipukizi, lakini wakiongozwa na Ben Blanco. Wengine ni Salma Juma, Peter Phimar, Kisegese, Kadogo, Dulla Said, Dogo Mandal, Julius Fred na wengineo wengi.

Baada ya kupata kibali kutoka serikalini, Blanco anaanza kazi ya kukusanya watoto mitaani kwa ajili ya kituo cha watoto yatima.

Haikuwa kazi rahisi. Ben Blanco alikumbana na changamoto nyingi kutoka kwa watoto hao kuanzia wa miaka mitatu hadi 17, ambao wengi walikuwa wameshazoea maisha ya kuzurura, kulala jalalani na kula chochote kinachopatikana. Ni maisha ambayo wamezoea, hivyo kwenda kukaa kwenye kituo ilikuwa mtihani mkubwa.

Waliopatikana maisha yao walianza kubadilika. Walianza kuwa wasafi kwa sababu ya kuoga mara kwa mara. Siha yao ilianza kubadilika, kwani walianza kunawiri. Ni kwa sababu walianza kula wanachokitaka na si wanachokipata. Pia walianza kusomeshwa. Hata hivyo bado baadhi ya watoto waliona hiyo ni kama kunyimwa uhuru wao. Walizoea kurura kutwa nzima wakitafuta wasichokijua wala kuwa na uhakika wa kukipata. Lakini walizoea maisha hayo, hivyo maisha ya kuchungwa, kukaa kutwa nzima wakisoma tu, wakila, kunywa kiulaini, kufanya kazi mbalimbali za kituo, waliona kama ni aina fulani ya utumwa.

Wengine walianzisha kampeni ya kutoroka ili wakaendelee na maisha yao ya zamani yaliyokuwa kama ndege. Walifanikiwa baada ya kumfungia msalani, watoto wakakimbia na kumuacha binti mwenye miaka mitatu, Kadogo ambaye alisalia na Blanco aliyekuwa akiwalea na kuwahudumia.

Maisha yao ya mara ya pili mitaani hayakuwa mazuri. Ni kwa sababu tayari walishaonja aina fulani ya maisha ya kuhudumiwa, kula wanachokitaka na hawazururi kusaka chakula.

Walianza kukonda. Kitendo cha kurejea tena mitaani, walipoteza muonekano wao na kuwa machokoraa yalioweza hata kutazamika.

Wote kwa ujumla waligundua makosa yao, wakajikusanya na kwenda kuomba radhi kwa Blanco wakiomba kurudishwa kituoni. Walikubaliwa na kuanza maisha mapya.





## Ayra unasema kulia ni dawa?

MWANAMUZIKI anayevuma nchini Nigeria, Ayra Starr, ametoa siri kwamba huwa analia kabla ya kupanda jukwaani kama njia ya kudhibiti hisia.

Katika mahojiano na kituo cha Cool FM, mwimbaji huyo amekiri kwamba mara nyingi anapata faraja moyoni kwa kulia na kusisitiza hali hiyo humkuta akizidiwa na hisia kali.

"Ninahisi kama ninalia kila wakati. Nina hisia sana, na napenda kulia dakika moja kabla sijapanda jukwaani," amesema



## Nicki Minaj maisha sawa na kitendawili

NYOTA wa muziki wa hip hop kutoka Marekani Nicki Minaj, licha ya kuwa mmoja wa wasanii wenye mafanikio, kumbukumbu zake za maisha ya utotoni humfanya kila mara kupata mfadhaiko.

Nicki Minaj, aliyezaliwa 1982 katika eneo la Onika Tanya Maraj Trinidad na Tobago, anakabiliwa na jinamizi kila anapokumbuka machungu aliyopata wakati akilelewa kwake na bibi yake na mateso ya mama yake kutoka kwa baba yake ambaye alikuwa anatumia dawa za kulevya.

"Kila mara amekuwa akipata shida akikumbuka maisha yake ya awali, aliishi katika mazingira magumu na wakati fulani alitaka kuwa mwigizaji ili apate pesa ya kumtunza bibi na mama yake," kimesema chanzo kimoja.


## Portable mwanamke ni pambo

MWANAMUZIKI wa muziki wa mitaa ya watu maskini nchini Nigeria, Portable, ameibua mjadala baada ya kumwita mpenzi wake wa zamani sawa na kifaranga cha kuku,

Katika mfululizo wa machapisho yake kwenye ukurasa wake wa Instagram, mwimbaji huyo wa kibao cha Zazu' ameonekana kukerwa na kitendo cha mwanamke huyo ambaye ni mama wa mtoto wao mmoja, kuonyesha kutokuwa na heshima wakati akifanyiwa mahojiano.

"Ni mahojiano gani yasiyo na maana ni kifaranga tu, mimi ni mwanaume mwenye majukumu nina mke nyumbani na watoto. Alipata mimba na nikakubali kulea mtoto, nimefanya vibaya?" amehoji Portable.





## Simi sijui kama utaeleweka!

MWIMBAJI maarufu wa Nigeria, Simi amesema ni muhimu kwa wapenzi kuanza kuishi pamoja kabla ya kufunga pingu za maisha.

Akitoa maoni yake kuhusu ndoa, msanii huyo amesisitiza kwamba maisha ya pamoja yataweka vipengele mbalimbali vya utu wa mtu kabla ya wawili kujitolea kwa ushirikiano wa maisha yote.

"Nishiriki maoni haya kwa sababu nadhani viongozi wa dini wanaweza wasikubaliane nami, lakini mimi binafsi nadhani kwamba watu wanaotaka kuoana wanapaswa kuishi pamoja kwa muda kidogo kabla ya kufanya hivyo," amesema katika maoni yake.

## Rita utawaokoa wengi

MWIGIZAJI wa Nollywood, Rita Edochie amewaonya Wanigeria dhidi ya unywaji pombe kupita kiasi na uvutaji sigara.

Nyota huyo katika filamu ya Mami Wata, katika ujumbewake kupitia ukurasa wake wa Instagram amesema kuna madhara mengi ya kiafya kutokana na unywaji wa pombe kupita kiasi na uvutaji sigara ambayo yanaathiri familia.

Edochie ameonyesha hofu yake kwa
wale wenye tabia hizo na kujiweka katika hatari ya kupata magonjwa ya figo, ini, moyo, na mapafu.





# Hakimu aagizwa kuhukumu wasiopeleka watoto shule

**Na Steven William,** MUHEZA

KATIBU Tawala wa Wilaya ya Muheza Tanga, Mohamed Mfaki amecharuka na kumuagiza Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya hiyo, Godfrey Haule kuandaa hukumu dhidi ya wazazi na walezi waliokaidi kupeleka shule watoto wao mwanzoni mwa mwaka huu.

Mfaki alitoa agizo hilo juzi wakati wa Kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Sheria nchini iliyofanyika viwanja vya Mahakama ya Wilaya ya Muheza vilivyopo Mtaa wa Mbaramo.

Alisema ameanza kuwachukulia hatua za kisheria wazazi na walezi wa watoto hao ambao wamekaidi agizo hilo halali la Serikali la kuwapeleka watoto wao kuanza elimu ya awali, msingi na kujiunga na kidato cha kwanza katika shule za serikali.

Mfaki alisema Hakimu Haule na wenzake, wanatakiwa kuandaa hukumu dhidi ya wazazi na walezi watakaofikishwa mahakamani wasomewe ili iwe fundisho kwao na kwa wengine wenye tabia kama hiyo ya kukwamisha mpango wa serikali wa kuhakikisha kila mtoto anapata haki yake ya msingi ya kuwa na elimu kwa manufaa yake ya baadaye.

"Ninataka kuona watoto wote wamepelekwa shule au wazazi wawe wamechukuliwa hatua za kisheria na nipate taarifa ya utekelezaji wa agizo hili," alisema.

Alionya kuwa hatavumilia kuona wazazi na walezi hao wakikwamisha juhudi za Serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwa imewekeza fedha nyingi katika ujenzi wa miundombinu ya shule na kuajiri walimu wa kutosha kuboresha elimu nchini.

Kwa upande mwingine, Mfaki aliwataka wananchi kuacha woga na kutumia mahakama kupata haki badala ya kumaliza mashauri kienyeji.

Aliwaomba watumishi wa mahakama kutenda haki kwa jamii katika kesi zao bila kuangalia hali yao ya kipato.

Katibu tawala huyo, alipongeza Serikali kwa kuboresha utendaji kazi wa mahakama nchini kwa kuweka mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwani unaharakisha usikilizaji mashauri kwa njia ya mtandao.

Hakimu Haule aliitaja changamoto inayoikabili Wilaya ya Muheza kuwa ni ukosefu wa gereza kubwa na uchakavu wa majengo ya mahakama za mwanzo na kuiomba serikali kuzitatua.

# Wapewa tahadhari wanaotibu macho kwa mkojo

**Na Oscar Assenga,** TANGA

DAKTARI bingwa wa macho wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga ya Bombo, Dk. Hussein Abbas Tayebji amewahadharisha wananchi kuepuka madhara kwa kutumia mkojo, maji yenye chumvi kutibu ugonjwa wa macho mekundu na kwenda hospitalini kupata tiba sahihi.

Tahadhari hiyo imekuja siku chache baada ya kuwapo kwa wimbi la ugonjwa wa macho mekundu kuendelea kuwakumba watu nchini.

Dk. Tayebji ambaye pia ni Mratibu wa Macho Mkoa wa Tanga, aliyasema hayo jana wakati akizungumzia hali ya ugonjwa huo kwa mkoa kuwa mpaka sasa zaidi ya watu 90 wameripotiwa kuupata, wengi wao wa Jiji la Tanga.

Aliwahimiza wanaokumbwa na ugonjwa huo kwenda vituo vya afya au hospitali kupatiwa matibabu na kuonokana na dhana potofu kuwa maji na haja ndoto ni tiba sahihi.

"Watu waache kutumia mitishamba, kuweka mkojo kwenye macho na maji ya chumvi kwa kufanya hivyo wanachotakiwa wafike kwa daktari kupata tiba sahihi," alisema

Aliwatahadharisha wananchi kuacha kushirikiana kwa matumizi ya taulo na vitambaa ili kuepukana na maambukizi ya ugonjwa huo.

Alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wanafunzi kujikinga na ugonjwa huo wanapokumbana na hali hiyo.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoa wa Arusha, Ally Juma (kulia), akishirikiana na wanachama wa jumuiya hiyo na wanafunzi wa Shule ya Msingi Burka, kupanda miti zaidi ya 117 kwenye kata ya Elerai, jijini Arusha juzi, ikiwa ni maadhimisho ya miaka 47 ya kuzaliwa kwa chama hicho. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Neema yawashukia waliohama Ngorongoro

**Na Hamida Kamchalla,** HANDENI

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Kanda ya Kaskazini imekabidhi mizinga 100 ya kufugia nyuki kwa vikundi vitatu vya mfano vya Kijiji cha Msomera wilayani hapa Mkoa wa Tanga.

Mizinga hiyo yenye thamani ya Shilingi milioni 10 imekabidhiwa kwa vikundi hivyo, Ewechena, Naiboshu na Datoga vya jamii ya wafugaji iliyohama kutoka eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro (NCAA).

Akikabidhi mizinga hiyo mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba wakati wa ziara yake ya kikazi kijijini hapo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi TFS wa Kanda hiyo, James Nshale, alisema moja ya majukumu ya wakala hao ni kuanzisha na kusimamia misitu ya hifadhi na hifadhi za nyuki.

"Tumeamua vikundi hivi vya mfano vitumie mizinga ya kufugia nyuki katika misitu hii ya hifadhi kama njia mojawapo ya kuhifadhi misitu.Huu ni mchango wetu kwao kama njia mbadala ya kuwaongezea kipato," alisema Nshale. Aliwaomba wanachama wa vikundi hivyo, wakazi wa kijiji hicho na wahifadhi wa misitu ya nyuki kuhakikisha misitu inalindwa kwa mujibu wa sheria za misitu na za ufugaji wa nyuki.

"Katika kuhakikisha tunafikia malengo tuliyokusudia mizinga hii itatundikwa katika maeneo hayo kwa kushirikiana na wataalamu wa misitu na nyuki pamoja na wanavikundi, pia tutaendelea kutoa elimu ya ufugaji nyuki na uhifadhi wa misitu kwa kushirikiana na wataalamu wa TFS na Halmashauri ya Wilaya ya Handeni," alisema. Akizungumza baada ya vikundi hivyo kukabidhiwa mizinga hiyo, Kindamba, alivitaka kutumia kuleta tija na kujiingizia kipato. Alisema Serikali imedhamiria kukifanya Kijiji cha Msomera kuwa cha mfano, hivyo ni imani yake wakazi hao watafanya shughuli za maendeleo ikiwemo ufugaji nyuki kuwaingizia kipato.

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Upinzani wa Msondo na Sikinde ulipoanzia

Na Adam Fungamwango



Msondo 1960

MSONDO Ngoma Music band, na Mlimani Park Orchestra mpaka sasa ndiyo bendi kongwe nchini na zenye upinzani wa jadi kama klabu za mpira wa miguu, Simba na Yanga.

Kama ilivyo kwa timu hizo za mpira lazima kuwe na kisa kilichotokea huko nyuma kilichosababisha Simba na Yanga ziwe na upinzani.

Siyo kwa timu hizo tu, hata klabu zingine zote duniani zenye uhasama haukuja tu hivi hivi. Kulikuwa na sababu.

Kwanza ikumbukwe kuwa bendi ya Msondo ilianza na jina na Nuta jazz kuanzia mwaka 1964 hadi mwaka 1977 ilipobadilishwa jina na kuitwa Juwata Jazz, baadaye Ottu Jazz na wakati wote huo ilikuwa inatumia mtindo wa Msondo Ngoma.

Orchestra Mlimani Park nayo iliyoanzishwa mwaka 1978, ilibadilishwa jina na kuwa DDC Mlimanin Park baadaye, kabla ya sasa kuitwa Mlimani Park Orchestra, nayo ikitumia mtindo wa Sikinde Ngoma ya Ukae.

Utajiuliza upinzani wa bendi hizi mbili umeanzia wapi? Ulianzia hapa.

Mwishoni mwa miaka ya 1970, wakati muziki wa dansi ukiwa kwenye chati ya hali ya juu, kulianza kuzuka wimbi la wanamuziki kuhama bendi moja na kwenda nyingine.

Hii haikushangaza sana kwa sababu, wanamuziki nao ni binadamu na wanatafuta maisha kama watu wengine. Lakini ilikuwa ikiwaumiza wapenzi na mashabiki wa bendi ambazo wanamuziki wanahama kiasi cha kukosa raha na amani.

Kwa upande wa wale ambao wamepata wanamuziki wapya inakuwa ni kicheko na furaha. Hata hivyo kwa jinsi ilivyokuwa ni kwamba hakukuwa na huzuni ya kudumu, pamoja na furaha ya kudumu kwa mashabiki na wapenzi wa bendi hizo.

Bendi zilizohusika sana kuchukuliana wanamuziki kwa mbinu zozote zile wakati huo ni Juwata Jazz Band, maarufu kama Msondo Ngoma, DDC Mlimani Park Orchestra, Orchestra Safari Sound, hasa ulipoingia mtindo wa Ndekule na Bima Lee, wakati wa mtindo wa Magnet Tingisha.

Pamoja na hayo, huwezi kuzungumzia bendi hizo kunya'ng'ana wanamuziki kama hujaitaja bendi ya Dar International. Hii ndiyo chimbuko la yote haya.

Ni hivi. Abel Bathazal, mpiga solo maarufu nchini wakati huo, alijiengua na bendi ya Msondo mwaka 1977 na kwenda kuunda bendi ya Dar International, akimchukua pia Marijani Rajab kutoka Safari Trippers, ingawa baadaye walikorofishana.

Mwaka 1978, Abel huyo huyo, baada ya kuhitilafiana na mmliki wa bendi, aliondoka na karibuni bendi nzima na kwenda kuunda bendi nyingine mpya, iitwayo, Mlimani Park Orchestra.

Tatizo ndipo lilianzisha hapa. Katika kuiboresha bendi, Mlimani Park ilikwenda Msondo na kumchukua Muhidini Gurumo ambaye alipofika aliipa jina la mtindo kuwa ni 'Sikinde Ngoma na Ukae.'

Kwa mashabiki wa Msondo lilikuwa ni pigo kubwa, lakini wakati wanaugulia maumivu, Sikinde ilirudi tena Msondo na kumkomba mwimbaji tegemeo, Hassan Bitchuka, mpiga saxophone, Juma Town na mpiga besi, Suleiman Mwanyiro.

Hili sasa likawa ndiyo pigo la mwaka kwa mashabiki wa Msondo. Likawagawa mashabiki wengi. Baadhi walihamia Sikinde kuwafuata Bitchuka na Gurumo. Wengine walibaki Msondo akiwa na majonzi. Hii ndiyo sababu kubwa ya bendi hizi kuwa mahasimu hadi leo hii.

Viongozi, wanamuziki na mashabiki wa Msondo, hadi leo wanaamini lengo wa Sikinde ilikuwa ni kutaka kuiua bendi yao ili wabaki wao tu kwa sababu bendi nyingi zilikuwa na wanamuziki wazuri tu, lakini wao waling'ang'ania kuwabomoa ili wasiwe na mpinzani kitu ambacho kinawauma hadi leo. Pamoja na kuchukuliwa wanamuziki Msondo baki ilibaki imara na kuwa bendi kubwa nchini, ya kuogopwa na inasadikiwa ndiyo inayoongoza kuwa na mashabiki wengi zaidi nchini, tena wa rika kufauti kuanzia miaka ya 1960, hadi 2000.

Kiasili kabisa, Dar Intenational ambayo iliondokewa na asilimia 90 ya wanamuziki kwenda kuunda Sikinde ndiyo ilitakiwa iwe bendi pinzani na Sikinde. haikuwa hivyo. Msondo 'iliununua' upinzani huo baada ya kuchukuliwa na vifaa vyake tegemezi.

Marijani aliyekuwa amesimamishwa kazi na Abel aliitwa na mmiliki, akaichukua Dar International kuisuka upya, baada ya wale walioondoka kwenda Sikinde, akaiita 'Super Bomboka'.

Sikinde iliendelea na tabia ya kwenda Msondo na kuchukua mwanamuziki yoyote ambaye iliona inamfaa.

Ndiyo maana iliwachukua pia, Shaaban Dede na Fresh Jumbe kwa nyakati tofauti wakati Msondo ikiwa imejiweka sawa. Kila Msondo ikikaa sawa, yenyewe inapeleka pigo.

Hata TX Moshi William, Joseph Lusungu, Abdul Ridhiwani, kama si nguvu ya mashabiki wa Msondo kuingia kati, huenda leo hii nao wangeingia kwenye historia hiyo ya kwenda Sikinde.

Kw upande wa Msondo, yenyewe ilikuwa ikichukua wanamuziki sehemu mbalimbali, ikiwemo Dar International kama vile Mustapha Hamisi 'Pishuu', Kakere Belesa, Kassim Mponda, Fresh Jumbe, Tino Masinge, Zitto Mbunda, Beto Julius na wengineo.

Kwa sababu asilimia kubwa ya wanamuziki wa Sikinde walitoka Dar International, iliaminika kuwa mwanamuziki yoyote wa bendi hiyo ana uwezo mkubwa, hivyo ilikuwa ni rahisi kupata kazi popote, ikiwemo Msondo.

Msondo walianza kupumua mwaka 1985, Ndala Kasheba alipoondoka OSS, na ili bidi isukwe tena, ndipo Gurumo, Bitchuka na wanamuziki kadhaa walipochukuliwa Sikinde kwenda kuimarisha bendi hiyo iliyokuwa na mtindo mpya wa Ndekule. Mashabiki wa wapenzi wa Sikinde nao wakaanza kuonja chungu ya kuchukuliwa wanamuziki.

Kama vile haitoshi walirudi tena na kumchukua Fresh Jumbe, Max Bushoke, Hamisi Juma 'Maalim Kinyasi' na kuweka chumvi juu ya kidonda.

Maumivu hayakwisha, kwani Bima Lee ilimchukua Dede, Joseph Mulenga, Abdallah Gama, Mwanyiro na wengineo. Hapo Sikinde ilipitia kwenye kipindi kigumu, huku Msondo ikipeta.

Hii inaitwa kla mtu na myonge wake. Msondo ilikuwa ni mnyonge wa Sikinde, lakini nao wakawa wanyonge kwa Bima Lee na Ndekule.

Ingawa wanamuziki hawa baadaye walikuwa wanazunguka kwenye bendi hizi hizi, mfano Gurumo na Dede walirejea na mauti kuwafika wakiwa Msondo, lakini hili la kuchukuliana wanamuziki, litabaki kuwa historia itakayoandikwa na kukumbukwa vizazi kwa vizazi, kwani ilikuwa ikileta upinzani, ubishi, burudani wakati mwingine ushindani mkali kwenye muziki wa dansi nchini.

Ukiwakuta mashabiki wa bendi hizi wakibishana ni kama watu wanaobishana mpira. Na pia miaka hiyo ya nyuma kuna wakati zinashindanishwa kwenye ukumbi. Hapo ndipo inapokuwa balaa. Watu wanafurika, muziki unapigwa na mshindi anapotangazwa inakuwa ni burudani ya aina yake.

Kila kitu kinatokea kwa sababu. Abel asingeunda Dar International, yote haya yasingetokea.

Asingekorofishana na mmiliki wa bendi ya Dar International na kuondoka na wanamuziki karibuni wote, Sikinde isingeundwa. Na kama isingeundwa, Msondo isingekuwa na bendi ya kuipa changamoto na kuwa moja ya bendi kubwa Afrika Mashariki.



DDC

## HABARI KIMATAIFA

# Marekani yakunjua makucha yaweka vikwazo kwa Israel

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imeanza kuonyesha makucha yake kwa Israel baada ya nchi hiyo kuwawekea vikwazo walowezi wanne wanaotuhumiwa kuwashambulia Wapalestina wanaoishi Ukingo wa Magharibi ambao inaikalia kwa mabavu.

Rais Joe Biden aliidhinisha vikwazo hivyo juzi kwa kutia saini amri ambayo pia inaeleza vitendo vya ghasia vinavyofanyika katika eneo la Ukingo wa Magharibi zimefikia viwango visivyovumilika.

Vikwazo hivyo ni pamoja na kuzuia mali zote za watu hao zilikuwa nchini Marekani pamoja na kifedha zilizohifadhiwa katika benki za nchi hiyo.

Ghasia katika Ukingo wa Magharibi zimeongezeka tangu Hamas ilipofanya mashambulizi dhidi ya Israel Oktoba 7 mwaka jana.

Kulingana na Umoja wa Mataifa, jumla ya Wapalestina 370 wameuawa katika eneo la Ukingo wa Magharibi tangu wakati huo. Wengi wao wameuawa na vikosi vya Israel na wanane kati yao wameuawa na walowezi.

Amri hiyo mpya imeonyesha misuli ya serikali ya Marekani kuwa ina uwezo wa kuwawekea vikwazo raia yeyote wa kigeni wanaoshambulia, kuwatisha au kunyakua mali ya Wapalestina.

Vikwazo hivyo ni vya kwanza kwa utawala wa Marekani na kuelezewa kama hatua adimu inayowalenga Waisraeli.

Wakati vikwazo hivyo vikitangazwa, Rais Biden alisafiri hadi jimbo la Michigan, ambalo wanaishi wakazi wengi wa Kiarabu na Wamarekani ambao wamekuwa wakikosoa uungaji mkono wake kwa Israeli.

Taasisi ya Kiarabu ya Marekani, ambayo inatetea haki za Wapalestina, awali ilisema tangu kuanza kwa mzozo huo, uungwaji mkono wa Wamarekani wa Kiarabu kwa Chama cha Democratic umeshuka kutoka asilimia 59 mwaka 2020 hadi 17 hadi sasa.

Wakati huo huo, jeshi la Israel limesema limesambaratisha kikosi cha Hamas katika eneo la Khan Younes.

Waziri wa Ulinzi wa Israel, Yoav Gallant alisema jeshi linazidisha mashambulizi yake katika mji huo ulioko kusini mwa Ukanda wa Gaza.

"Tunakamilisha misheni zetu huko Khan Younes. Pia tutafika Rafah na kuondoa vikosi vya kigaidi vinavyotutishia," alisema Gallant.

Raia wengi wa Palestina walikimbilia kusini mwa Ukanda wa Gaza na kisha kutakiwa kuelekea Rafah kutokana na mashambulizi makubwa kutoka kwa vikosi vya Israel.

Hapo awali vikosi vya nchi hiyo vililenga kwa kutumia mashambulizi ya mabomu na ardhini katika eneo la kaskazini ambako wanaishi Wapalestina milioni 2.3.Mji wa Rafah, ambako ni kivuko pekee cha mpaka wa Misri na Ukanda wa Gaza usiodhibitiwa na Israel, umekuwa njia kuu ya kupeleka misaada ya kibinadamu katika eneo hilo tangu kuanza kwa vita hiyo.

Katika hatua nyingine, kiongozi wa Hamas, Ismaïl Haniyeh, anatarajiwa kuwasili nchini Misri kushiriki mkutano wa kutafuta mapatano mapya na Israel katika mapigano yanayoendelea Ukanda wa Gaza.

Chanzo kimoja kimelieleza shirika la habari la AFP kwamba Hamas ilikuwa inapitia pendekezo la kusitisha vita kwa wiki sita katika vita vyake na Israel.

Hatua hiyo inakuja baada ya wapatanishi kukutana nchini Ufaransa kwa ajili ya kutafuta njia ya usitishaji wa mapigano kati ya pande hizo mbili.

**BBC**

## Wakulima Ufaransa wasitisha mgomo

**PARIS,** UFARANSA

VYAMA vya wafanyakazi wa kilimo nchini Ufaransa vimetoa wito wa kuondoa vizuizi barabarani baada ya Waziri Mkuu, Gabriel Attal kutangaza kuunga mkono sekta hiyo ambayo imezorota kutokana na kuibuka kwa mgogoro.

"Kwa kuzingatia kila kitu kilichotangazwa tunahitaji kubadilisha njia zetu za utekelezaji wa mgomo na kwa hiyo tunatoa wito kwa mitandao yetu kusitisha vizuizi na kuingia katika aina mpya ya uhamasishaji", alisema mkuu wa wakulima vijana, Arnaud Gaillot.

Pia mwenyekiti wa muungano wenye nguvu wa wakulima (FNSEA) Arnaud Rousseau, alikaribisha hatua hiyo kwa kueleza inaonyesha maendeleo yanayoonekana.

Vyama vya wafanyakazi viliweka masharti kadhaa ya kukomesha maandamano ikiwamo kupitishwa kwa sheria ya mwelekeo wa kilimo kwa siku zijazo pamoja na kuweka angalizo nchi za Ulaya hadi mwezi Juni.

"Ikiwa matakwa haya hayatafikiwa kufikia hadi mwezi Juni, hatutasita kuingia tena mitaani," alisema Arnaud Gaillot.

**RFI**



Matrekta yaliyotelekezwa na wakulima yakifunga barabara kuu ya Longvilliers karibu na jiji la Paris kama sehemu ya mgomo wao kupinga hatua ya serikali kuondoa ruzuku. **PICHA: REUTERS**

# Mlipuko waua watatu na 270 kujeruhiwa Kenya

**Nairobi,** KENYA

WATU watatu wamekufa na wengine 270 wamejeruhiwa baada ya lori lililobeba mitungi ya gesi kulipuka nchini Kenya.

Tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia jana katika mtaa wa Embakasi ulioko jijini Nairobi.

Mlipuko huo umesababisha hali ya majonzi kutanda nchini humo kutokana na kuleta hasara sehemu kubwa ya mtaa huo pamoja na raia kupata hofu kutokana na moto mkubwa ulioambatana na moshi mzito.

Kulingana na taarifa ya jeshi la polisi la nchi hiyo,mlipuko huo ulisababishwa na mitungi ya gesi iliyopakiwa kwenye lori kuwaka moto na kisha kuteketeza maghala na makazi ya watu yaliyokuwa karibu na eneo la tukio.

Mkazi mmoja aliyejitambulisha kwa majina ya Alfred Juma, alisema alimshauri dereva wa lori asiwashe lakini hakumsikiliza.

"Nikaamsha watu ili wasiungue, nikamwendea dereva wa lori kumshauri asiwashe gari, lakini hakunisikia alipowasha gari lenyewe, mitungi ya gesi ikalipuka. Moto ukashika majengo."

Moto huo pia uliteketeza magari kadhaa na mali za biashara, ikiwa ni pamoja na majengo ya biashara.

Hata hivyo, raia wengi wanahoji kwa nini mabohari ya gesi yamejengwa karibu na makazi ya watu.

"Kwa kweli hii kitu haistahili wasingejenga kwenye eneo la makazi ya watu, kama haingejengwa mbali tusingepata maafa kama haya," aliongeza kusema.

Kati ya majeruhi hao, 21 wanatibiwa katika hospitali ya Taifa ya Kenyatta, 160 wamepelekwa katika Hospitali ya Mama Lucy, 19 katika Hospitali ya Mbagathi, 14 katika Hospitali ya Modern Komarock na wanane katika Hospitali ya Nairobi West.

Daktari Martin Wafula, ambaye ni Ofisa mkuu mtendaji wa Hospitali ya Mama Lucy alisema walipeleka magari ya wagonjwa 15 kutoa huduma kwa watu walioathirika.

Msemaji wa serikali Isaac Mwaura alisema kuwa eneo lililotokea ajali hiyo limefanyiwa uchunguzi na kuonekana ni usalama, na kituo kimeanzishwa kusaidia kuratibu operesheni za uokoaji na huduma nyingine muhimu kwa waathirika.

**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**ANDERSON ELISONGUO SARIAH** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 687 ALZ. ENGINE NO H20A117434. CHASSES S NO TDIIW108582**. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. Taarifa ya polisi: PHQ/ARU/ARU/1517/2024.

## SHERIA YA UANDIKISHAJI WA ARDHI (SURA 334) KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO

**MMILIKI ALIYEANDIKISHWA:** RAMADHANI JUMA HANTE
**ARDHI:** KIWANJA NA. 49 KITALU 'HH' ENEO LA CHANG'OMBE
**MWOMBAJI:** ASHA SANDA HALLO

**TAARIFA IMETOLEWA,** Kwamba barua ya toleo iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa hati Milki mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa siku thelethini (30) tokea tarehe ya taarifa hii itakapotagazwa katika gazeti la serikali/ magazeti ya kawaida yaliyopo kwenye jamii.

**BARUA YA TOLEO NAKALA HALISI** ikionekana, irudishwe kwa:

**Mkurugenzi,**
**Halmashauri a Jiji,**
**P.O. BOX 1249,**
**DODOMA.**

Imetolewa na:
Ibunga J.J
Afisa Ardhi Mteule
**DODOMA,**

**29 Jnanuary, 2024.**

## KUPOTEA KWA NYARAKA YA UMILIKI KIWANJA

Halmashauri ya Manispaa Mtwara/Mikindani inatangaza kupotea kwa barua ya miliki ya kiwanja Na. 10 Kitalu **"BB" CHUNO** Mtwara ya Ndugu **THABITI AHMADI THABIT** Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **AHMAD MOHAMED** wa S.L.P 92 Mtwara.
Kwa yeyote atakayeiona awasiliane ndani ya siku 30 katika Ofisi za Ardhi.
Kwa yeyote aliyenayo au mwenye pingamizi au atayeiona awasilishe ndani ya siku 30 katika Ofisi za Ardhi.
Vinginevyo baada ya siku 30, Ofisi itatoa nakala ya Nyaraka ya umiliki na kuendelea na hatua stahiki za kisheria. Taarifa ya Polisi: **PHQ/MTW/MTW/308/2024.**

STAHIKI ZA KISHERIA.
Mpangala P.N
Kny: MKURUGENZI WA MANISPAA
MANISPAA YA MTWARA/MIKINDANI

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**SUMMONS BEFORE THE COMMISSION FOR MEDIATION AND ARBITRATION**
**(HATI YA WITO MBELE YA TUME YA USULUHISHI NA UAMUZI)**
**((Made under regulation 34(1)) (Imetengenezwa Chini ya Kanuni ya 34 (1))**
**Labour Dispute No. (Mgogoro wa kikazi Na.) CMA/DSM/ILA/677/2023**
**Between/Baina ya**
**BAKARI SEFU MASANGA.............Applicant (Mlalamikaji/Mwombaji)**
**And/Na**
**MEDTRONIC AG...............Respondent (Mlalamikiwa/Mjibu Maombi)**
**NOTICE TO ATTEND MEDIATION/ARBITRATION HEARING**
**(TAARIFA YA KUITWA KUHUDHURIA KWENYE SHAURI LA USULUHISHI/UAMUZI)**

Take notice that the above mentioned Mediation/Arbitration has been fixed hearing on ...day of...yeare 2024 at.... Hours, at **DAR ES SALAAM ZONE, AKIBA-BITI TITI ROAD** (Unaarifiwa kuwa shauri lililotajwa hapo juu, linalokuja kwa hatua ya usuluhishi/Uamuzi, limepangwa kusikilizwa tarehe 26 Mwezi 02 Mwaka 2024 saa 4:00 asubuhi.
You are required to appear before the Commission in person and or accompanied by on Advocate/Personal representative as instructed and produce on that day all relevant documents you intend in rely upon in support of your defence. You are further cautioned to remain in attendance until permitted by the Commission (Unatakiwa kufika binafsi ama kwa kuambatana na wakili/Mwakilishi wako mbele ya Tume kama ulivyoagizwa. Unapaswa kuleta vielelezo/nyaraka muhimu unazo kusudia kuzitumia katika utetezi wako. Unatahadharishwa usipuuze kutii wito huu na unatakiwa kubakia kwenye majengo ya Tume mpaka utakapo ruhusiwa kuondoka na Tume).
Given under my hand and Seal of the Commissioin this... day of.... Year 2024(Imetolewa na kugongwa muhuri wa Tume leo tarehe 01 Mwezi 02 Mwaka 2024.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA RUFAA YA MADAI NA.292 YA 2023**
**JUSTINE F.BUFURE ...............MRUFANI**

**DHIDI YA**
**HAJI R. MWIKALO ...................MJIBU RUFANI NA.1**
**JACK PEMBA.........MJIBU RUFANI NA.2**
**KWA: JACK PEMBA**

### POPOTE ULIPO

Unajulishwa kwamba shauri la rufaa ya Madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na Mahakama hii hapa Dar Es salaam tarehe 14/2/2024 saa tatu kamili asubuhi(9:00).
Unapaswa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hautahudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayetambulika kisheria basi rufaa itasikilizwa bila ya uwepo wako.
Imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 19/1/2024

THE COURT OF APPEAL OF TANZANIA
A. S. CHUGULU
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA YA RUFANI

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**VICENT JACKOB BUTIKU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 795 CUC aina ya NISSAN CIVILIAN. Chassis namba RYW40010942. Engine namba TD42EAA0942. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIN/15869/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ELIRAMSON PAUL MBISE**
Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya pikipiki(HAOJUE) yenye namba za usajili MC 887DND, Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu nayeye. **PHQ/MOR/MOR/2456/2024**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTE KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**

**OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.
Mob: +255 - 0677020701
E-mail: advertise@guardian.co.tz,
Website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

# MAMA MWENYE NYUMBA - 13

MWANTUMU, au mama Mwadawa, ni mwanamke ambaye muda wote yeye anachowaza ni umbea, ugomvi na kufitinisha watu. Anawagombanisha majirani wasielewane, ndoa za majirani zake nazo haziko salama hajaziacha, kwani amekuwa akizitikisa. Kwa bahati mbaya au nzuri anaishi kwenye nyumba ya urithi ya marehemu mama yake, yeye akiwa ndiye mama mwenye nyumba. Cheo hicho cha Umama wa Nyumba asiyojenga, ndiyo akawa amepata fimbo ya kuwapigia watu. Wapangaji wanaopanga kwenye nyumba hiyo wamekuwa wakiishi kwa amri, manyanyaso, kufokewa kama watoto wadogo. Ndani ya nyumba hiyo, wapangaji wamekuwa kama wakiishi bure au kwa mama wa kambo, huku silaha yake kubwa ikiwa ni kuwatishia kuwahamisha. Hebu fuatilia mwanzo na mwisho wa visa vya mama huyu.

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

"Umeanza na wewe, kama huna la kusema kata simu hiyo."

Yalikuwa ni mazungumzo ya simu ya mtu na binti yake. Mwantumu na binti yake Mwadawa.

Mwantumu akiwa nyumbani kwake, Mwadawa kwa mjomba wake Gongolamboto wakipeana dondoo na kile kilichotokea siku ya fumanizi na nini kinaendelea baada ya hapo.

Wapangaji waliobaki Rozi na Tabia ni kama walibaki wakiwa. Kitendo cha Devota kuondoka ilikuwa pigo kubwa kwao.

Pamoja na hayo hata wao walikuwa karibuni kuondoka kwenye nyumba hiyo. Ila, awali walipatana kuwa hata wakihama, watakapopata nyumba za kuhamia, angalau wasiwe mbalimbali sana na wala wasihamie mbali sana na pale.

Lengo ni kuendeleza vita nyingine na Mwantumu, mama mwenye nyumba wao kwa sasa.

Walijua kuwa watakapokuwa nje ya utawala wa nyumba yake, watampelekesha kweli kweli.

Kama tu wapo kwenye nyumba yake na wanamkosesha usingizi, basi watakapokuwa wamepanga sehemu nyingine, hawatotishika na amri zozote za umama mwenye nyumba, badala yake atakuwa kwao ni mtu wa kawaida tu.

Katika mazungumzo yao, Tabia ya Rozi wakaamua kumfuata Devota Kawe kuongea naye kwa jambo moja tu, la kulipiza kisasi cha mama mwenye nyumba wao.

**********************************

Kazi kubwa na nzuri ambayo Tabia na Rozi waliyoifanya ni kumtuliza mpangaji mwenzao Devota.

Walipofika Kawe kwa shangazi yake walimuweka kitako na kumwashauri asiivunje ndoa yake kwa ajili ya mama mwenye nyumba wao Mwantumu na biti yake Mwadawa.

Mwanzo haikuwa rahisi, lakini baadaye akalainika. Mumewe Jonas akapigiwa simu. Akaja yakazungumzwa na hatimaye Peter na mkewe wakarudiana.

Tayari Jonas alikuwa ameshapanga chumba maeneo ya Kinondoni Biafra. Akamchukua mkewe na kuanza tena maisha mengine.

Hapo moja kwa moja walikuwa wameshahama. Kilichofanyika tu kwa msaada wa Tabia ya Rozi, walifanya kila njia ikiwemo kwenda kwa mjumbe ambaye aliamua chumba chao kifunguliwe na vyombo vya vichukuliwe.




**Kitu ambacho hakukijua Bishada ni kwamba maneno yote aliyokuwa akiongea Mwantumu ni ya uongo.**

Jonas alikutana na mjumbe na kumueleza kuwemo na vyombo kwenye chumba chake na kuwateua akinadada wale wawili wapangaji wenzake kuvisimamia kupakiza kwenye gari na vipelekwe kwake.

Ndipo Mwantumu alipopata taarifa kuwa Jonas na mkewe Devota wamehamia Kinondoni Biafra.

Alimsikia dereva akiongea na utingo wake siku walipokuja kuchukua vyombo kuwa vinakwenda huko.

Katika upekepeke wake anagundua kuwa Jonas na mkewe wamerudiana. Ikamuuma sana. Kwa sababu alidhani huenda akaachwa Devota na binti yake akachukua nafasi.

Siku hiyo akaenda kwa shoga yake Bishada.

"Bora umekuja shoga unifungefunge mabutu kwanza, maana nywele zimefumuka hizo."

"Tena bora maana leo nina ubuyu ndugu yangu, umenikaa hapa!"

"Na wewe Mwantumu kwa ubuyu, ndiyo maana unasutwa kila kukicha shoga yangu."

"Bila umbea nalala ndugu yangu, yaani utanikereketa hadi niutoe."

Bishada alikuwa tayari ameshatoa kiti nje ya nyumba yake. Yeye mwenyewe akakaa kwenye mkeka.

Ususi ukaanza huku kila mmoja akiwa na dukuduku moyoni. Bishada akawa ana hamu ya kutaka kusikia ni kitu gani ambacho anataka kuambia.

Mwantumu yeye alikuwa anatafuta anapangilia tu maneno kichwani aanze na lipi anamalizie lipi.

"Enhe mwezangu sasa nikwambie. Yule mpangaji wangu aliyehama."

"Devota?"

"Huyo huyo, si unakumbuka jinsi walivyohama?"

"Si tangu siku ile alivyomfumania mumewe na binti yako?"

"Ndiyo si hajarudi tena hadi leo na juzi wale wapangaji wangu vichefuchefu wakamsaidia kutoa vyombo vyake."

"Ndiyo nimeambia hilo."

"Sasa shoga yangu Bishada mwanzo walikuwa wametengena, sasa hivi wamerudiana."

"Mwantumu, wale hawakuachana, wamefunga ndoa Kanisani, ila mwanamke alikwenda kukaa kwao kwa hasira tu. Na nikwambie usichokijua, hao hao wapangaji wako ndiyo wamewapatanisha."

"He Bishada, kumbe na wewe umo ee, yote haya umeyajuaje?"

"Ukijua huu wenzio nao wanajua huu!" Bishada akampasha shoga yake.

"Basi dada sasa hivi wanaishi Kinondoni Biafra."

"Wamepanga?"

"Wapange wapi? Wanakaa nyumba ya tajiri mmoja. Wao wameambia wailinde."

"Toba, ndiyo hivyo? Mbona nimeambia wamepanga nyumba nzuri tu, siyo kama kibanda chako, ina bomba, ila maji humo humo!"

"Wapi, wapi dada, habari zao zote ninazo, pesa ya kupanga chumba hawana, kuna mtu kawaonea huruma kaamua kuwaweka kwenye nyumba yake ili walinde."

"He makubwa."

"Mimi nililijua hili wakitoka kwangu hawawezi kupata sehemu kama yangu, bwana mwenyewe nasikia bodaboda yenyewe sasa hivi mbovu, pesa hana."

"Sasa Mwantumu maneno yote hayo yanakutoka, ukivyotaka kumpachika binti yako itakuwaje?"

Kitu ambacho hakukijua Bishada ni kwamba maneno yote aliyokuwa akiongea Mwantumu ni ya uongo.

Alikuwa akieleza maneno hayo kwa ajili ya chuki kwa sababu pamoja na yote yaliyotokea, bado Jonas amepatana na mkewe.

"Na nasikia juzi tu dada, mvua imenyesha maji hadi shingoni. Wamelala wima. Eneo hilo kumbe lina mafuriko, mbona kazi wanayo. Wamejifanya kuondoka kwangu hakula lolote walilofanya. Wamekwenda kukaa nyumba ya bure kama wako bweni vile, na mafuriko juu."

"Isije tu ukawa unawasagia kunguni kumbe uongo!"

"Mtu aliyenipa data namumini Bishada, na hatahangaika sana kwa sababu baada ya hayo mafuriko kseho yake bwana kaenda kulala kwa ndugu zake, bibi huyo karudi huko huko kwa shangazi yake Kawe. Wanasubiri kukauke warudi tena hapo hapo. Wangebaki kwangu yote haya yangewapata kweli? Nyumba mbovu ndiyo lakini hakuna mafuriko."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# COASTAL UNION YAJIPANGA, OUMA AKIIOTA 'NNE BORA'

**Na Oliver Albert**

COASTAL Union inatarajia kukutana na 'ndugu zao' African Sport katika mechi ya kirafiki itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga imeelezwa.

Mbali na kuimarisha vikosi cha timu hizo mbili kuelekea lala salama, mchezo huo wa kirafiki ni maalumu kwa ajili ya kuadhimisha miaka 47 ya kuzaliwa kwa Chama cha Mapinduzi (CCM).

Coastal Union itarejea tena katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara Februari 12, mwaka huu itakaposhuka ugenini kuikabili KMC kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

**Kocha Mkuu wa Coastal Union, David Ouma, alisema kikosi chake kilitumia vyema mapumziko ya ligi kujiimarisha na anatarajia watarejea kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa na 'nguvu kubwa'.**

Ouma alisema wanatarajia kucheza katika kiwango bora katika kila mechi kwa sababu malengo yao ni kumaliza msimu huu kwenye nafasi nne za juu.

Alisema anaamini maingizo mapya katika dirisha dogo yataongeza ubora ndani ya kikosi chake na atahakikisha wanatimiza malengo yao ya kufanya vizuri katika Ligi Kuu pamoja na mashindano ya Kombe la FA.

"Tunaendela vizuri na mazoezi kujiandaa na ligi na kwa sababu tumeona bado tuna mda mrefu kabla ya mechi yetu ijayo dhidi ya KMC, tumeaona tucheze mechi ya kirafiki ili kujiweka sawa.

Wachezaji tuliowaongeza kikosini naamini wataongeza chachu ya timu kufanya vizuri zaidi, bado hatujaridhika na nafasi tuliyopo, tunahitaji kupanda juu zaidi na naamini tunaweza kwa sababu hakuna mwenye nafasi yake kwenye msimamo wa ligi, " alisema Ouma.

Kocha huyo amewataka wachezaji wake kuendelea kupambana ili kuhakikisha malengo waliyojiwekea msimu huu yanatimia.

Coastal Union imewaongeza kikosini Salim Aiyee, Crispin Ngushi huku pia ikiwapandisha nyota wengine watano kutoka timu ya vijana.

Kikosi hicho kiko katika nafasi ya sita kwenye msimamo wa ligi kikiwa na pointi 19 baada ya kucheza michezo 14, imeshinda mechi tano, imetoka sare michezo minne na kupoteza mitano.




Meneja Biashara wa Tigo, Fabian Felician (kushoto), na Ofisa Habari wa Betika, Juvenalius Rugambwa (kulia), wakiwa na mshindi wa televisheni wa Kampeni ya Twende Zetu Ivory Coast Ki-VIP, Maulid Mohamed jijini, Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Twende Zetu yakabidhi televisheni

**Na Mwandishi Wetu**

WASHINDI wengine wawili, Maulid Mohammed wa Mkuranga na Ramadhani Issa kutoka Lindi wamekabidhiwa zawadi ya televisheni za inchi 70 kila mmoja zinazotolewa na Betika na Tigo katika hafla iliyofanyika jijini, Dar es Salaam jana.

Akizungumza jijini jana, Ofisa Habari wa Betika Tanzania, Rugambwa Juvenalius, alisema wanaendelea kutoa zawadi hizo kwa washindi hadi Februari 11, mwaka huu shindano hilo litakapomalizika rasmi.

Juvenalius alisema hadi wanafunga droo hiyo, Betika kwa kushirikiana na Tigopesa watakuwa wametoa jumla ya televisheni 14 zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 17.

"Shindano bado linaendelea, wateja wanatakiwa kuweka pesa yake katika akaunti ya kubashiri ya Betika kupitia Tigopesa na mshindi atakuwa amepata TV ya inchi 70, ambayo ataitumia kwa shughuli mbalimbali ikiwamo kumwingizia kipato kwa kuonyesha mipira katika vibanda umiza, " Juvenalius alisema.

**Akizungumza jijini jana, Ofisa Habari wa Betika Tanzania, Rugambwa Juvenalius, alisema wanaendelea kutoa zawadi hizo kwa washindi hadi Februari 11, mwaka huu shindano hilo litakapomalizika rasmi.**

Aliongeza washindi wa Twende Zetu Ivory Coast Ki-VIP waliokwenda kuishangilia Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), iliyokuwa inashiriki Fainali za 34 za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2023) nchini humo wamerudi nyumbani.

Stars ilitolewa katika hatua ya makundi huku Morocco na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) zikisonga mbele kutoka Kundi F.

# Kipanga wajiandaa kuibania Malindi SC

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WANAJESHI wa Kipanga FC wanashuka wanatarajia kuwakabili wakongwe Malindi katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa leo kuanzia saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Mau A.

Katika mzunguko wa kwanza timu hizo zilitoka sare ya bila kufungana wakati Malindi ndio alikuwa mwenyeji wa mchezo huo.

Kipanga FC wanashuka uwanjani wakiwa katika nafasi ya tano kwenye msimamo wa ligi hiyo wakati wapinzani wao Malindi wako nafasi ya 13.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Hassan Abdulrahman, alisema mchezo huo utakuwa mgumu tofauti na unavyoangaliwa na mashabiki wa soka la Zanzibar.

Alisema wanakutana na timu nzuri na yenye uzoefu mkubwa katika Ligi Kuu Zanzibar hivyo amejipanga kutumia mbinu ya kushambulia ili kuhakikisha wanapata alama tatu muhimu.

"Mara nyingi unapokutana na timu inayohitaji kujinasua na hatari ya kushuka daraja lazima mchezo huo huwa mgumu na wenye kuzidiana mbinu ili kila mmoja apate alama tatu," alisema kocha huyo.

# Gofu kushindana kutafuta viwango

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya wazi ya gofu (Northern Zone Championship) yamepangwa kufanyika kuanzia Februari 9 hadi 11, mwaka huu kwenye viwanja vya TPC Moshi mkoani, Kilimanjaro.

Shindano hilo linafanyika kwa mara ya kwanza na linatambuliwa rasmi na World Amateur Golf Ranking (WAGR).

Akizungumza na Nipashe jana, nahodha wa klabu hiyo, Jaffar Ally, alisema shindano hilo linafanyika kwa mara ya kwanza likiwa na lengo la kuwapima wachezaji wa Tanzania kuingia kwenye orodha ya viwango vya kimataifa.

Ally alisema shindano hilo litachezwa kwa mashimo 54 ambapo mshindi wa jumla atazawadiwa kitita cha sh. milioni moja huku pia kutakuwa na washindi kwenye makundi mengine ya Division B, C, vijana na wanawake.

Aliongeza pia kutakuwa na mashindano ya mashimo 36 yatakayofanyika kati ya Februari 10 na 11, mwaka huu huku akisema usajili utafungwa Februari 6.

## ZISIKUPITE

### BENZEMA KUBAKI SAUDIA
MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Karim Benzema, alihusishwa kuondoka Al-Ittihad Januari, lakini atafanya mazungumzo ya wazi na klabu hiyo ya Saudia ambayo inataka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 abaki kwa msimu mwingine. (***Ben Jacobs***)

### CHAMBERS AWEKA MSIMAMO
MLINZI wa Aston Villa, Calum Chambers alikataa ofa kutoka timu tatu za Championship, licha ya klabu hiyo ya Midlands kuwa tayari kumruhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 kuondoka. (***Football Insider***)

### BROM ILIMTAKA CHAMBERS
WEST Brom ilikuwa ni moja ya klabu zilizotaka kumsajili beki wa zamani wa Arsenal, Calum Chambers. (***Mail***)

### LOOKMAN ANUKIA JUVENTUS
WINGA wa zamani wa Everton, Ademola Lookman, mwenye umri wa miaka 26, analengwa na Atletico Madrid na Juventus, ambao wanaweza kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa Nigeria, ambaye kwa sasa anachezea Atalanta. (***Sun***)

### WEST YAMGOMEA BENRAHMA
KLABU ya West Ham ilikataa mpango wa mkopo wa dakika za mwisho mwisho kutoka kwa Fulham kwa winga wa Algeria, Said Benrahma, mwenye umri wa miaka 28. (***Fabrizio Romano***)

### HAMILTON KUTA UNITED
NYOTA wa Formula 1, Lewis Hamilton, ambaye atajiunga na Ferrari mwakani, tayari amedokeza anaweza kuungana na Sir Jim Ratcliffe katika klabu ya Manchester United mara tu pazia la ushirikiano wao na Mercedes litakapofungwa baadaye mwaka huu. (***Express***)

### LOKONGA MAMBO MAZURI
KLABU ya Arsenal inaweza kumpa kiungo wa kati wa Ubelgiji, Albert Sambi Lokonga, nafasi nyingine baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 kufanya vyema akiwa kwa mkopo Luton Town.(***Football Transfers***)

### GILL AFURAHISHWA SPURS
WINGA wa Hispania, Bryan Gil, alikuwa akihusishwa na uhamisho wa mkopo Januari lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 ameamua kubakia Tottenham Hotspur. (***Fabrizio Romano***)

### SENSI HAKIJAELEWEKA CITY
UHAMISHO wa mkopo wa kiungo wa kati wa Italia, Stefano Sensi, kutoka Inter Milan kwenda Leicester City umezimwa licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kufaulu vipimo vya afya hapo juzi. (***Telegraph***)

### SELS AJIUNGA FOREST
KLABU ya Nottingham Forest imemsajili mlinda lango wa Ubelgiji, Matz Sels, kutoka Strasbourg ya Ufaransa ya Ligue 1 kwa ada ya takriban pauni milioni tano. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 amejiunga kwa mkataba wa miaka mitatu na nusu.(***BBC Sport***)

### UNAL RASMI BOURNEMOUTH
KLABU ya Bournemouth imemsajili mshambuliaji wa Uturuki, Enes Unal, kwa mkopo kutoka Getafe. Unal mwenye umri wa miaka 26, amefunga mabao 36 katika mechi 109 katika timu hiyo ya LaLiga tangu ajiunge nayo kutoka Villareal mwaka 2020. (***BBC Sport***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BELLINGHAM: MADRID IMENIBORESHA KIWANGO

**MADRID,** Hispania

●●● Mshambuliaji huyo avunja rekodi ya Alfredo, Cristiano katika...

JUDE Bellingham amesema kucheza kwenye Uwanja wa Bernabéu kunakufanya "ajisikie kama mchezaji mzuri" alipotafakari miezi yake sita ya kwanza akiwa Real Madrid, na kuongeza anatumaini kudumisha kiwango chake katika klabu hiyo kwa "misimu mingi ijayo."

**Bellingham amefunga mabao 18 katika mechi 26 akiwa na Madrid msimu huu tangu ajiunge nayo akitokea Borussia Dortmund majira ya joto yaliyopita.**

"Siku zote unajua Real Madrid ndio klabu kubwa zaidi duniani," alisema Bellingham akiiambia Real Madrid TV.

"Lakini basi ni tofauti tu unapopata uzoefu. Hasa Bernabéu, ni jambo la kushangaza tu. Unahisi mtu mkubwa sana. Ni poa sana, huelewi jinsi klabu ilivyo kubwa."

"Hakuna mahali popote unapoweza kwenda ambapo watu hawakutambui. Wakati mwingine ni jambo zuri na wakati mwingine ni jambo baya," aliongeza Bellingham.

"Unatambua tu ni hatua hiyo darasani, katika kila kitu kweli. Lakini pia mgeuko unapoingia mazoezini kila siku, wachezaji huwa watulivu sana, kocha ni mtulivu sana. Ni mazingira mazuri ya kufanya kazi."

Kiwango cha Bellingham akiwa na Madrid kimemfanya kushinda Tuzo ya Golden Boy mwaka 2023 ya Mchezaji Bora wa Ulaya chini ya umri wa miaka 21, pamoja na taji la Ballon d'Or, tuzo ya mwanasoka bora zaidi duniani wa chini ya umri wa miaka 21.

Alianza maisha kwa kuvunja rekodi nchini Hispania, akifunga mabao 14 katika mechi 15 za kwanza za Madrid, na kuipita idadi ya magwiji wa klabu, Alfredo Di Stefano na Cristiano Ronaldo.

"Ninahisi niko nyumbani," alisema Bellingham.

"Familia yangu iko vizuri. Nimekuwa na marafiki ambao wamefurahia sana jiji. Mashabiki wana heshima sana, wananitendea vizuri, jambo ambalo ninashukuru sana.

"Nimefurahishwa sana na mwanzo. Ni kuhusu kuudumisha sasa kwa msimu mmoja, na misimu mingi ijayo, katika klabu hii kubwa."

Madrid wanakabiliwa na mfululizo wa michezo mwezi huu ambayo inaweza kubainisha msimu wao. Wanawakaribisha Atlético Madrid kwenye LaLiga Jumapili, kabla ya kucheza na Girona ugani Bernabéu mnamo Februari 10, na kufuatiwa na mechi yao ya mkondo wa kwanza ya hatua ya 16 ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya RB Leipzig siku tatu baadaye.

"Siku zote ni muhimu kucheza kibinafsi, lakini haijalishi ikiwa timu haishindi," Bellingham alisema. "Kuona hilo hadi sasa tuko kileleni katika LaLiga, tukiwa na kombe moja tayari na kilele cha kundi letu la Ligi ya Mabingwa... hadi sasa, ni nzuri sana.

## HABARI MICHEZO

# USHINDI WA UNITED WAMVURUGA TEN HAG



**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag alikiri alikuwa na "hisia mseto" baada ya Manchester United kupoteza uongozi wa mabao mawili dhidi ya Wolves, lakini wakashinda 4-3, shukrani kwa bao la dakika za lala salama la Kobbie Mainoo.

Mainoo alifunga dakika ya 97 kwenye Uwanja wa Molineux na kushinda mchezo huo dakika mbili tu baada ya Pedro Neto kufikiria ameipa Wolves pointi moja kwa kufanya matokeo ya sare ya 3-3.

United walitawala kipindi cha kwanza na walionekana kama mchezo huo ni kama wameumaliza.

"Nina hisia tofauti," alisema Ten Hag.

"Upande mmoja, umefurahishwa sana. Bila shaka ni ushindi mkubwa na nadhani kwa shabiki wa upande wowote, mtazamaji wa mchezo huu, ilikuwa nzuri kuona.

"Lakini kama kocha, unapoona unatawala mchezo kwa saa moja, unapaswa kwenda 3-0 au 4-0 kwa saa, halafu jinsi tunavyoruhusu mabao tunapaswa kusimamia vizuri zaidi uwanjani."

Mainoo alikuwa shujaa wa United baada ya kiungo huyo mwenye umri wa miaka 18 kujipenyeza kwenye eneo la hatari na kufunga bao lake la kwanza katika Ligi Kuu England.

Marcus Rashford pia alizifumania nyavu baada ya kurejeshwa kwenye timu kufuatia adhabu yake kwa 'kujirusha' kwenye klabu ya usiku ya Belfast wiki iliyopita kabla ya kuiambia timu alikuwa mgonjwa sana na hawezi kufanya mazoezi.

"Unaona roho ya timu na uimara na haswa kwa Kobbie Mainoo, hiyo ni nzuri kuona," alisema Ten Hag.

"Tuna tabia sahihi, roho kwenye chumba cha kubadilishia nguo ni nzuri sana unapoweza kuonyesha hili. Nadhani timu nzima ilicheza vizuri sana."

Hata hivyo, kwa sifa zote walizotundikiwa Mainoo na Rashford, Ten Hag pia aliitaja timu yake kuwa "wajinga" baada ya kuwa mbele kwa 2-0 na 3-1 kabla ya kurudishwa kwa 3-3.

"Tulipaswa kusimamia mchezo vizuri zaidi," alisema Ten Hag.

"Lazima tuondoe makosa haya, hayawezi kutokea. Tulikuwa na hatua nyingine kwenye michezo ya msimu pia. Kinachoulizwa ni uongozi na haiwezi kutokea kwamba unaruhusu mabao kama haya"

# Msaidizi wa Klopp afunguka

**LIVERPOOL,** England

KOCH msaidizi wa Liverpool, Pep Lijnders, ametoa wito kwa klabu hiyo kufuta pazia la enzi ya Jurgen Klopp na kumalizia "ngoma ya mwisho" na kuongeza kundi la makocha lilihisi muda wao kwenye klabu ulikuwa unakaribia mwisho msimu uliopita.

Klabu hiyo ya Merseyside ilithibitisha wiki iliyopita Lijnders na makocha wenzake wasaidizi ,Peter Krawietz na Vitor Matos wataungana na Klopp kuondoka Liverpool mwishoni mwa msimu huu.

Watatu hao wamekuwa washiriki wakuu wa Klopp na kocha huyo wa Ujerumani hivi majuzi aliangazia mchango wa Lijnders na jukumu ambalo amecheza katika kutekeleza mtindo wa soka wa Liverpool.

"Sio rahisi kuacha klabu kama hiyo. Lakini katika maisha nahisi lazima ufanye jambo sahihi na jambo sahihi inamaanisha kwenye majira ya joto tulisema tunaendelea na tunaenda na kila kitu tulicho nacho, tunaifanya kuwa ya Mwisho," alisema Lijnders katika mahojiano na tovuti ya Liverpool.

"Bila kujua ingekuwa msimu huu, lakini nilijua mradi unakaribia mwisho. Nilihisi kwa umiliki wa umiliki, kusajili wachezaji wanaofaa, tunarudi kwenye misingi."

Lijnders, ambaye alijiunga na klabu hiyo mwaka wa 2014 kama kocha wa akademi ya vijana, alianza kujihusisha na kikosi cha kwanza baada ya kuteuliwa kwa Klopp mwaka uliofuata na alichukua jukumu muhimu katika maendeleo ya wahitimu wa akademi akiwamo, Trent Alexander-Arnold.

Kocha huyo raia wa Uholanzi aliondoka Liverpool mwanzoni mwa 2018 na kuchukua mikoba ya NEC Nijmegen lakini baada ya muda mfupi wa miezi mitano nchini Uholanzi Klopp alimpa nafasi ya juu katika timu yake na kumrejesha klabuni hapo.

Katika kipindi hicho, Liverpool wameshinda mataji sita, ikiwa ni pamoja na Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2019 na Ligi Kuu England mwaka uliofuata.

"Yeye ni Klopp, rafiki, kakai. Tumepitia mengi hapa: nyakati nzuri, nyakati mbaya. Nina imani kamili, tunaaminiana kikamilifu, ndiyo sababu inafanya kazi," alisema.

"Jinsi anavyonipa uhuru wa kuongoza timu, kubuni mafunzo, kufanya maamuzi ya kimbinu, ambayo inasema kila kitu. Inasikitisha kwamba tunaenda lakini ninafurahi kwa kile kilicho mbele."

# Broja wa Chelsea atua Fulham




**LONDON,** England

ARMANDO Broja amekamilisha uhamisho wake wa mkopo kutoka Chelsea na kujiunga na Fulham hadi mwisho wa msimu huu.

Maelezo ya kifedha ya mpango huo hayakufichuliwa lakini vyanzo viliiambia ESPN Fulham italipa ada ya mkopo ya pauni milioni nne kwa kijana huyo wa miaka 22.

Chanzo kimoja kiliongeza ada ya mkopo itashuka hadi sifuri ikiwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Albania ataanza mara 10 kwa Fulham.

"Nimefurahi sana tumefikia makubaliano ya kumleta kwa mkopo Armando Broja kwa Fulham hadi mwisho wa msimu. Ni mshambuliaji mchanga na mwenye kipaji ambaye ana furaha na ari ya kujiunga na kikosi chetu," alisema Mkurugenzi Mtendaji wa Fulham, Tony Khan.

Broja ameichezea Chelsea mechi 19 katika michuano yote msimu huu, akifunga bao lake pekee la Ligi Kuu England dhidi ya Fulham Oktoba, mwaka jana na jingine kwenye mechi ya raundi ya tatu ya Kombe la FA dhidi ya Preston North End, mwezi uliopita.

Kocha wa Chelsea, Mauricio Pochettino, alisema mwezi uliopita mshambuliaji huyo angekuwa na sehemu muhimu ya kuichezea timu yake bila ya Nicolas Jackson, ambaye alikuwa ugenini na kikosi cha Senegal kwenye fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON).

Broja alikuwa sehemu ya kikosi cha Chelsea kilichofungwa 4-1 na Liverpool Jumatano iliyopita, ingawa hakucheza.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 atakuwa nyongeza ya kukaribishwa kwa Fulham ambayo imefunga mabao 28 pekee katika michezo 22 ya Ligi Kuu England.

Kikosi cha Marco Silva kitashuka tena dimbani leo katika mechi ya Ligi Kuu kumenyana na Burnley.

HABARI MICHEZO

# SERENGETI GIRLS, FUTSAL KAZINI ZAMBIA, NAMIBIA

**Na Saada Akida**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17, (Serengeti Girls) inatarajia kukutana na wenyeji Zambia katika mechi ya kwanza ya kusaka tiketi ya kufuzu fainali zijazo za Kombe la Dunia (U-17) itakayochezwa leo mjini Lusaka.

Serengeti Girls inashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kufuzu kwa mara ya kwanza fainali zilizopita za michuano hiyo zilizofanyika India mwaka juzi, ikiishia hatua ya robo fainali.

Timu hizo zitarudiana Jumamosi ijayo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Serengeti Girls, Hilda Masanche, alisema baada ya kuwasili salama Zambia walipata muda mzuri wa kuendelea na maandalizi ya mchezo huo na sasa wachezaji wake wako tayari kwa mechi hiyo.

Masanche alisema ameendelea kuwakumbusha wachezaji mbinu mbalimbali na mpango wanaotakiwa kuutumia katika mchezo huo ili kufikia malengo ya kupata ushindi.

Aliongeza anafurahi kuona uelewa wa nyota wake umekuwa mzuri na kila mchezaji anaonekana kuwa tayari kupambana ili kupata matokeo chanya katika mechi hiyo.

"Vijana wetu wapo na mapambano ya kuwania nafasi ya kufuzu, nina kikosi bora, tumeandaa timu katika nafasi zote ikiwamo safu ya ulinzi na ushambuliaji kulingana na ubora wa wapinzani wetu (Zambia)," alisema kocha huyo.

Wakati huo huo, Timu ya Taifa ya Futsal itashuka dimbani leo kuvaana na wenyeji Namibia kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika.

Mkuu wa msafara wa timu hiyo, Issa Bukuku, alisema wachezaji wako katika hali nzuri na kilichobaki ni kusubiri muda wa mchezo huo ambao utachezwa katika mji wa Windhoek.

Katika hatua nyingine Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), imepangwa Kundi A katika mashindano ya All Africa Games yatakayofanyika Machi, mwaka huu jijini Accra, Ghana.

Twiga Stars imepangwa pamoja na Uganda, Ghana na Ethiopia huku Kundi B likiwa na Morocco, Senegal, Nigeria na Algeria.




Msemaji wa Kampeni ya Magifti Dabodabo, Haji Manara (kushoto) akimkabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni tano, Monalisa Kasonta jijini, Dar es Salaam jana baada ya kuibuka mshindi katika droo ya wiki hii kwenye promosheni hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Monalisa, Swai washindi magifti*

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAZI wa Dar es Salaam, Monalisa Kasonta na Hemed Swai jana waliibuka washindi wa sh. milioni tano kila mmoja katika droo ya wiki hii ya promosheni ya magifti dabodabo inayoendeshwa na Kampuni ya Tigo.

Mbali na hao, Eliva Eliazaro, aliibuka mshindi wa Sh. milioni moja huku Ismail Rashid akiibuka mshindi wa vifaa vya nyumbani ambavyo ni friji, televisheni, microwave na redio ya kisasa wakati akimchagua baba yake mdogo, Iddi Maulidi, kuwa mshindi mwenza ambaye naye alipewa vifaa hivyo.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa fedha zake, Monalisa, alisema hakuamini alipotangazwa mshindi katika droo hiyo iliyochezeshwa Jumatano iliyopita na kuishukuru Tigo kwa kuwajali wateja wake.

Naye Ismail alisema kwake yeye hiyo ni zawadi kubwa ambayo itaendelea kuwa kumbukumbu nzuri kwake.

"Nilikuwa na ndoto ya kumiliki vifaa kama hivi, nashukuru kupitia Tigo ndoto yangu imetimia, nawashukuru sana Tigo kwa kweli," alisema Ismail.

Msemaji wa promosheni hiyo, Haji Manara, alisema promosheni hiyo iliyoanza Novemba mwaka jana inaelekea ukingoni na kuwataka wateja wa Tigo kuchangamkia fursa kwa kushiriki kufanya miamala mbalimbali ili kupata nafasi ya kushinda.

Manara alisema katika droo ya mwisho watatoa zawadi ya magari mapya kwa wateja watakaoshinda.

# Usajili wa Msimbazi waitisha Geita Gold

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Geita Gold, Denis Kitambi, amesema usajili wa dirisha dogo uliofanywa na Simba utaufanya mchezo wa Ligi Kuu Bara utakaowakutanisha Februari 12, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza kuwa mgumu kwao.

Akizungumza jana mjini Morogoro ambako wameweka kambi, Kitambi, alisema maingizo mapya katika kikosi cha Simba yamewachanganya, hasa kwenye benchi la ufundi.

"Tulijua tutacheza dhidi ya Simba, kikubwa ni sisi tunahitaji pointi tatu kwa sababu tunacheza tukiwa nyumbani, lakini changamoto ninayoiona kuelekea katika mchezo huo ni mpinzani amefanya usajili mpya, kwa hiyo inabidi uangalie hayo maingizo mapya wana ubora gani, wanachezaje kitu ambacho hatuwezi kufahamu kwa sasa, tunakwenda kucheza na baadhi ya wachezaji ambao hatuwafahamu vyema," alisema Kitambi.

Kocha huyo alisema kitu pekee anachotegemea ni mechi tatu (Mashujaa FC, Tabora United na Azam FC) kabla ya kucheza na Simba watazitumia kujiimarisha na kuongeza mbinu.

Katika dirisha dogo la usajili, Simba imewaongeza Boubacar Sarr, Salehe Karabaka, Omar Jobe, Freddy Michael, Ladack Chasambi na Edwin Balua.

# TECNO yakabidhi viatu 300, Karia awashukuru

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), limepokea viatu vya kuchezea seti 300 kati ya 1,000 wanazotarajia kupata kutoka katika Kampuni ya Simu ya TECNO kwa ajili ya Timu ya Soka ya Taifa ya Umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), imefahamika.

Rais wa TFF, Wallace Karia, alisema jana katika makabidhiano hayo, anawashukuru TECNO msaada huo na kutambua mchango wa shirikisho hilo na serikali katika juhudi za kukuza soka kwa kusaidia vijana.

Karia alisema viatu hivyo vitaenda kwa kambi ya vijana zaidi ya 50 ambayo inaingia kambini leo jijini, Tanga ikiwa ni sehemu ya mradi wa TFF katika kukuza soka nchini.

"Milango ipo wazi kwa kampuni zote, nawashukuru TECNO na nawaomba walete mabango yao katika vituo vya Kigamboni na Tanga ili nao waonekane kama wamesaidia vijana, tunawashukuru na kuwaombea katika biashara zenu," alisema Karia.

Balozi wa TECNO, Burton Mwambe 'Mwijaku', alisema kampuni hiyo inasaidia watoto wenye vipaji kwa kuwapa nyenzo mbalimbali ili kutimiza ndoto zao.

Nipashe
# Michezo
Jumamosi Februari 3, 2024




Bellingham: Madrid imeniboresha kiwango UK. 21




Kiungo wa Yanga, Khalid Aucho (kulia), akijiandaa kumtoka nyota wa Kagera Sugar Mzambia, Obrey Chirwa katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba jana. Timu hizo zilitoka suluhu. **PICHA: MTANDAO**

# Yanga yabanwa 'mbavu' Kaitaba

## ●●● Yaambulia suluhu na Kagera, yaifikia Azam FC lakini...

**Na Saada Akida**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wameshindwa kutamba ugenini baada ya kulazimishwa suluhu na Kagera Sugar katika mchezo wa ligi hiyo uliochezwa kwenye Uwanja wa Kaitaba ulioko Bukoba mkoani, Kagera.

Matokeo hayo yanaifanya Yanga kufikisha pointi 31 sawa na Azam FC huku Mashujaa yenyewe ikibakia katika nafasi ya 15 kwenye msimamo wa ligi hiyo baada ya kufikisha pointi 10, Mtibwa Sugar yenye pointi nane inaendelea kuburuza mkia.

Yanga walifanikiwa kutawala mchezo huo lakini wachezaji wa Kagera Sugar walicheza kwa nidhamu na kuwaheshimu mabingwa hao watetezi na kufanikiwa kugawana pointi dhidi ya wenyeji hao wa Jangwani, Dar es Salaam.

Safu ya ushambuliaji ya Yanga kama ingekuwa na utulivu kutokana na kufika mara kwa mara langoni kwa wapinzani wao ingepata mabao, lakini walinzi wa Kagera Sugar walijipanga imara kuondoa mipira ya hatari.

Yanga walitawala mchezo katika dakika 45 za kwanza kwa kutumia muda mwingi kucheza kwenye eneo la mpinzani, lakini utulivu wa Kagera Sugar uliwasaidia kuzuia mianya ya wageni hao kwa kuwabana kila walipokuwa na mpira.

Kagera Sugar yenyewe ilifanya mashambulizi yake kwa kushtukiza ambapo walifanikiwa kufunga bao ambalo lilikataliwa na mwamuzi wa kati, Ally Simba, kutoka Geita baada ya kutafsiri mfungaji alikuwa katika eneo la kuotea.

Mwamuzi huyo pia alimwonyesha kadi ya njano nyota wa Kagera Sugar, Deogratius Mafie, dakika 45 baada ya kumchezea rafu Pacome Zouzoua, Deus Bukenya na Ally Nassor (84') aliyemchezea vibaya, Shekhan Ibrahim wa Yanga.

Kiungo Mganda wa Yanga, Khalid Aucho, dakika ya 56 alipoteza nafasi nyingine baada ya kushindwa kuunganisha mpira wa faulo uliopigwa na Pacome Zouzoua na kuwafanya mashabiki wao waendelee kutulia wakisubiri goli.

Yanga ilifanya tena shambulizi lingine dakika ya 69, Pacome akijaribu kupiga shuti lakini kipa wa Kagera, Ramadhani Chalamanda aliudaka mpira na kuwanyima wageni hao bao huku dakika 59, Ally Ramadhani wa Kagera Sugar alikosa nafasi wazi kwa kupiga shuti dhaifu lililopanguliwa na kipa wa Yanga, Metacha Mnata.

Chalamanda alifanya kazi nzuri dakika ya 90 baada ya kucheza shuti kali lililopigwa na Kennedy Musonda ambaye alikuwa katika nafasi nzuri ya kuifungia bao Yanga.

Yanga : Metacha Mnata, Yao Koussi, Nickson Kibabage, Gift Fred, Dickson Job, Aucho, Max Nzengeli/ Malatse Makudubela 'Skudu' , Salum Aboubakar 'Sure Boy'/ Shekhan Ibrahim (dk 33), Clement Mzize/ Joseph Guede, Pacome na Farid Mussa/ Kennedy Musonda (dk 57).

Kagera Sugar: Ramadhani Chalamanda, Datius Galiwango, Abdallah Mfuko, Deus Bukenya, Abdallah Seseme, Ally Nassor, Ally Ramadhani, Obrey Chirwa, Mbaraka Yusuph na Deogratius Mafie.

Nyota wa Kagera Sugar, Mfuko, alisema matokeo hayo yametokana na wao kufuata maelekezo ya benchi la ufundi la kuhakikisha wanawazuia Yanga kuondoka na alama tatu katika mechi hiyo.

"Tuliona ubora wa Yanga na kufanyia kazi, tuliweza kuzuia mashambulizi na tumefanikiwa kupata alama moja," alisema Mfuko.

# Simba yawaandalia mtego Mashujaa FC

**Na Saada Akida**

WAKATI imemrejesha kikosini kiungo wake wa kimataifa kutoka Zambia, Clatous Chama, Simba inatarajia kuwavaa wenyeji Mashujaa FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani, Kigoma.

Chama amerejea kikosini baada ya uongozi kumsamehe makosa yake ya utovu wa nidhamu, lakini uamuzi wa kucheza leo utakuwa chini ya Kocha Mkuu, Abdelhak Benchikha, ambaye leo atamkosa beki, Henock Inonga, anayeitumikia Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) kwenye Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), zinazoendelea huko Ivory Coast.

Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, aliliambia gazeti hili mechi hiyo haitakuwa rahisi kutokana na timu hiyo kuiwahi kuwaondoa katika mashindano ya Kombe la FA miaka ya nyuma, lakini leo anaimani kuna mabadiliko makubwa katika timu yao.




Matola alisema Mashujaa ni timu mpya na ina mwalimu mpya lakini wamejipanga tofauti kuwakabili na wako tayari kukabiliana na ushindani watakaokutana nao lakini malengo yao makubwa ni kuondoka na alama tatu muhimu.

"Tunajua watakuja kupambana ili wapande juu katika msimamo wa ligi, lakini pamoja na ugumu wa mechi tutahakikisha tunapata matokeo chanya na kwenda kwenye mechi ijayo tukiwa na alama tatu kutoka kwa Mashujaa FC.

Chama ni kweli amejiunga na timu leo (jana), ni jambo zuri kwa sababu ni mmoja mwa wachezaji muhimu, suala la kucheza hili ni juu yetu kama benchi la ufundi nani acheze na asicheze katika mchezo huu kulingana na mipango yetu," alisema Matola.

Aliongeza mabadiliko waliyofanya katika safu ya ushambuliaji ni kawaida katika kikosi yakiwa na lengo la kutengeneza uimara akisema pia ni ngumu kuweka wazi kuhusiana na nyota wapya waliosajiliwa kwa kuwatazama kupitia mechi moja ingawa anaimani kubwa wataisaidia timu.

Naye Kocha wa Mashujaa FC, Abdallah Mohamed 'Bares', alisema anatambua Simba ni timu kubwa, lakini anakikosi imara na anakiamini.

Alisema kikosi chake kimerekebisha makosa mbalimbali yaliyokuwapo na hivyo leo anatarajia kuona mchezo mzuri kutoka kwa wachezaji wake.

"Tumejiandaa kupata matokeo mazuri mbele ya Simba, naamini kila mmoja anatambua umuhimu wa pointi tatu, hivyo tutapambana kuzipata," alisema kocha huyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >